# Nipashe

Jumanne Machi 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580521

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**DPP** aagiza kukamatwa kwa waendesha upatu

UKURASA 2



**Wajawazito** watabika kukosa wodi ya kujifungulia

UKURASA 7

**Cavani, Martial kuiwahi AC Milan**

UKURASA 20

# Samia: Tushikamane zaidi kipindi hiki

• **Awasilisha** salamu za JPM, akisema...*Endelea ukurasa 2*



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo katika kiwanda cha kuchakata mahindi Michungwani, Segera, wilayani Handeni mkoani Tanga kutoka kwa Meneja Mtendaji wa kiwanda hicho, John CK jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MGOMO DALADALA WAITIKISA MBEYA**

SHUGHULI za usafiri na usafirishaji katika Jiji la Mbeya...

UKURASA WA 4

**MOTO WATEKETEZA MABWENI SHULENI**

MOTO mkubwa ambao chanzo chake bado hakijafahamika, umeteketeza jengo lenye...

UKURASA WA 5

**OFISA ARDHI KORTINI UHUJUMU UCHUMI**

WATU watatu wakiwamo mpima ardhi na mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Nahukukahuka...


**Benki Kuu yakamilisha elimu usajili wa VICOBA**

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Mbaroni tuhuma kumiliki heka 10 shamba la bangi

UKURASA 3


**MICHEZO** **SIMBA: MERRIKH HAWATOKI LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia: Tushikamane zaidi

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka Watanzania kupuuza maneno yanayotoka nje na kuwahakikishia kuwa Tanzania iko salama.

Aidha, aliwataka wananchi waendelee kushirikiana na kushikamana kuijenga nchi yao.

"Katika kipindi hiki kama mnavyosikia kwenye nchi yetu maneno ni mengi, mengi sana, na hayatoki ndani, mengi yanatoka nje, nataka kuwahakikishia kwamba tuko salama na kubwa tushikamane na kushirikiana," alisisitiza.

Makamu wa Rais alisema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mkata, wilayani Handeni, mkoani Tanga baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa jengo jipya la halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema nchi iko salama na kuwataka kuendelea na dua, kuchapa kazi ili kuijenga Tanzania yao. Akiwa katika eneo hilo la Segera, aliwapa salamu za Rais John Magufuli.

"Mheshimiwa Rais anawasalimia sana na anawashukuru sana sana sana, kwa kazi nzuri mliyoifanya mwezi wa kumi mwaka jana ya kurejesha Serikali ya Chama Cha Mapinduzi madarakani, mmefanya jambo jema kwa sababu sasa tunakwenda kukamilisha yale ambayo tuliyoyaahidi kwenye ilani nayo ni ni haya hapa tunayaona kwa macho yetu pamoja na mengine na mengine," alisema Samia.

"Kwa hiyo Rais anawasalimia sana anasema tuko salama, tuchape kazi, twende vizuri, tujenge upendo na mshikamano wa Watanzania ili taifa letu likue liwe na tija zaidi."

Akiweka mawe ya msingi katika viwanda viwili mkoani humo, aliwapongeza wananchi kwa kupata kiwanda cha mazao ya nafaka ambacho alisema kitatatua kilio cha cha siku nyingi cha wakazi wa eneo hilo.

"Niwapongeze kwa kuwa na kiwanda hiki, hiki ni mkombozi, nilipokuwa nakuja nilifikiri ni kiwanda kidogo tu, lakini nimeingia na kusikiliza maelezo ya mwekezaji kumbe ni kiwanda kikubwa sana," alisema Samia.

"Nakumbuka kipindi cha kampeni cha 2010 nilipokuja kulikuwa na kilio kikubwa cha machungwa kuozea barabarani, sasa huu ndio usuluhishi wa kilio hiki, tumeleta umeme, maji na ndiyo maana kiwanda hiki kipo hapa."

"Tanzania ina sera ya uchumi wa viwanda, tunakwenda kwenye uchumi mkubwa lakini kupitia kwenye viwanda, naomba sana mlinde viwanda hivi kwa sababu vitatoa ajira kwa wenyeji wa maeneo haya. Tumepata utatuzi wa kilimo chetu ambacho siku nyingi kilituliza, nawasihi acheni hujuma kwenye viwanda vinavyokuja katika maeneo yenu."

Samia alitoa wito kuhakikisha kwamba a kati ya ajira 600 zinazotarajiwa kupatikana katika kiwanda hicho, robo mbili ya ajira za kawaida zitolewe kwa wananchi wa kawaida katika eneo hilo.

Akizungumzia mradi huo, Samia alisema mpango wa sasa wa serikali ni kuhakikisha inafikisha huduma zote muhimu karibu na wananchi.

Mradi wa jengo hilo ambalo limefikia asilimia 40 ya ujenzi, umetumia Sh. milioni 200 na linakadiriwa kugharimu Sh. bilioni 5.3.Mradi huo unagharamiwa na serikali na halmashauri inatekeleza kwa kutumia mafundi jamii.

Matumizi ya mafundi hao, yamesaidia kuokoa kiasi cha Sh. milioni 591.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Willium Makufwe, alisema kuwapo kwa kamati za ujenzi katika mradi huo kumesaidia kuwaletea wananchi huduma muhimu karibu.

"Tunaishukuru serikali kutuletea mradi huu, italeta tija sana kwao kuunda kamati ambayo imeshirikisha viongozi wote wa halmashauri katika kufanikisha ujenzi, kamati tulizounda ni ujenzi, manunuzi, utunzaji wa vifaa, mapokezi na ufuatiliaji na zinasimamia majukumu waliyopewa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alisema mkoa umepokea zaidi ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya halmashauri yapatayo matatu ambayo ni Handeni Mji, Handeni Vijijini na Bumbuli huku akieleza kuwa ni hatua mbalimbali za ujenzi uliofikiwa.

Hata hivyo, wananchi walitoa kero ya umeme kukatika wakati wa kazi jambo ambalo linawagharimu na kuwapa hasara katika uzalishaji hasa katika sekta ya viwanda vidogo vidogo pamoja na wafanyabiashara wa eneo hilo ambalo wanafanya kazi zao usiku.

Akizungumzia suala hilo, Samia alisema mpaka ifikapo muda wa serikali kutoka madarakani itakuwa imepiga hatua kwa kumaliza kero nyingi zilizopo kwa kipindi kirefu na kwamba ipo haja ya kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa suala hilo linapatiwa ufumbuzi.

***Imeandikwa na Hamida Kamchalla (Handeni) na Elizabeth Zaya (Dar)***

# DPP aagiza kukamatwa wanaoendesha upatu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP) Biswalo Mganga, ameviagiza vyombo vya dola kuwakamata na kuwahoji wanaojihusisha na biashara ya upatu.

Aidha, amepiga marufuku vyombo vya upelelezi kurudisha fedha kwa watu walioshiriki kwenye makosa ya michezo ya upatu.

DPP Biswalo amesema utaratibu wa kurejesha au kutaifisha mali kwa waathirika zinazohusiana na uhalifu umeainishwa kwenye sheria mbalimbali ambapo vyombo vya upelelezi vinatakiwa kuufuata.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Mganga, alisema kuwa katika siku za hivi karibuni kumekuwa na wimbi la udanganyifu wa fursa za uwekezaji kutoka kwenye baadhi ya taasisi zikiwaaminisha wananchi kujiunga na michezo ya upatu na kupata faida zaidi kwa kipindi kifupi.

Aidha, alisema kuwa mipango hiyo inafanyika pasipo kupata idhini ama vibali kutoka kwenye mamlaka za serikali, huku taasisi zinazofanya biashara hiyo zikiwa hazina ofisi rasmi zinazotambulika katika uendeshaji wa shughuli zao.

Alisema michezo hiyo ni makosa ya jinai na ni ukiukwaji wa masharti ya Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha Namba Tano ya Mwaka 2006, inayokataza mtu yoyote kupokea miamala ya fedha kutoka kwa umma bila leseni.

Alisema pia michezo hiyo ya upatu imekuwa na madhara makubwa kwa wananchi ambao wamekuwa wakiingia bila kujua wanakwenda kupoteza fedha zao.

Pia alisema serikali imefanikiwa kutaifisha kiasi cha fedha ambazo zilitumika katika upatu ambapo wakati wa Dec walitaifisha kiasi cha Sh. bilioni 16, yakiwamo magari pamoja na nyumba.

"Pia tumetaifisha kiasi cha Sh. bilioni 500 kwa kampuni ya D9, Mr Kuku bilioni 5 na Rifaro bilioni tatu hadi 4," alisema.


**INVENTURE MOBILE TZ LIMITED**

**Cheti cha usajili namba 116266**

Sheria ya makampuni, 2002

(KIFUNGU 334 (1))

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha Inventure Mobile TZ Limited (kampuni), yenye usajili namba 116266, kilichofanyika tarehe 10 October 2020 azimio maalumu lilipitishwa:

1. kufuatana na kifungu 331 (1) (b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. wanahisa wamemteua Joseph Lyimo wa Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelatini (30). Madai yote yafungwe ndani ya bahasha na yatumwe kwa JOSEPH LYIMO wa PricewaterhouseCoopers Limited ya Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania, ambaye ni mfilisi wa kampuni. Maombi yote yatakayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa..

……………………………………

**JOSEPH LYIMO**

MFILISI wa INVENTURE MOBILE TZ LIMITED


# Walalamikia operesheni kamata nyama kuwaingiza hasara kilo 400

**Na Christina Mwakangale**

WAFANYABIASHARA wa nyama katika machinjio ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam, wamesema wamepata hasara ya kilo zaidi ya 400 baada ya operesheni ya kukamata nyama zinazouzwa kwa mafungu iliyofanywa na Bodi ya Nyama Tanzania.

Bodi ya Nyama Tanzania, juzi, ilipiga marufuku uuzaji wa nyama kwa mafungu katika maeneo ya nje ya machinjio ya Vingunguti kutokana na kuhatarisha afya ya mlaji.

Kufuatia tukio hilo, Idara ya Mifugo na Uvuvi jijini Dar es Salaam, imeondoa marufuku hiyo hadi ujenzi wa bucha mpya utakapokamilika.

Mwenyekiti wa Ushirika wa Wafanyabiashara ya Mifugo na mazao yake, Joel Meshack, akizungumza kwenye kikao kilichokutanisha viongozi wa ushirika, serikali na wafanyabiashara wa eneo hilo, alisema lengo la kukutana ni kuzungumzia operesheni ya kukamatwa kwa nyama hizo jana.

Pia alisema kuwa pamoja na mambo mengine ajenda ya namna ya kupata vifungashio ama mifuko mbadala kwa ajili ya kubebea nyama vilivyosajiliwa na serikali.

Alisema mkutano huo uliandaliwa na wafanyabiashara hao uliwashirikisha viongozi wa serikali wakiwamo maofisa mifugo, Jeshi la Polisi ili kupata muafaka wa biashara ya nyama hizo.

Meshack alisema mradi wa ujenzi wa bucha mpya ambao haujakamilika, ulipaswa kuwa subira kwa sasa kwa bodi kuruhusu biashara hiyo kufanyika kwa sababu eneo lililotengwa awali kuwa dogo.

"Rais wetu ametuelekeza kuishi na umoja, kitendo cha kuchoma nyama zilizokamatwa haikuwa busara, tunazalisha shilingi bilioni moja kila mwaka," alisema Meshack.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi Jiji la Dar es Salaam, Andrea Majaliwa, aliwataka wafanyabiashara hao kuwa wavumilivu wakati ujenzi wa vyumba vya kuuzia nyama ukiendelea na kuwataka waendelee na biashara yao.

Meya wa Manispaa ya Ilala, Omar Kumbilamoto, alisema amesikitishwa na tukio hilo na kwamba machinjio hiyo ilikuwa inaingiza Sh. milioni 100 kwa mwezi kabla ya Septemba mwaka 2019, Rais John Magufuli, kusitisha kutozwa kwa ushuru eneo hilo.

Kumbilamoto alisema, Rais Magufuli alitoa agizo hilo ikiwa ni kutoa nafasi ya maboresho ya machinjio hayo.

HABARI KITAIFA

# Mbaroni kwa tuhuma za kumiliki shamba la bangi

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

JESHI la Polisi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga linawashikilia watu wawili Kijiji cha Kalole, Halmashauri ya Msalala kwa madai ya kumiliki shamba la bangi na ghala la kuhifadhia bangi hiyo.

Watuhumiwa hao wametajwa kuwa ni Nding'wa Masinde (54), mkazi wa Kijiji cha Kalole na Yohana Bula (25), mkazi wa Tabora Itumbo, ambao walikamatwa kwenye msako uliofanywa na Jeshi la Polisi na kukutwa wakimiliki shamba hilo lenye ukubwa wa hekari 10.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kalole, Nyawaminza Migabe, watu hao walikamatwa kwenye operesheni hiyo kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji hicho ya kuwabaini watu wote wanaojishughulisha na uuzaji wa dawa za kulevya aina ya bangi.

Migabe alisema katika msako huo walimkamata Charles Lubiwa, akiwa na misokoto ya bangi na baada ya kuhojiwa alitaja mahali alikoitoa na mmiliki wa shamba hilo.

Alisema kuwa baada ya kumkamata mmiliki wa shamba hilo aliyejulikana kwa jina moja la Masinde, waliwajulisha wananchi wa kijiji hicho kuwa mtuhumiwa huyo ni mkulima mahiri wa zao hilo haramu. Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kulima mazao haramu badala yake wajikite katika mazao halali kama mahindi, mpunga na viazi ambavyo vinaweza kubadili maisha yao.

Migabe alisema, katika eneo la Kijiji cha Kalole, wenyeji wengi wanajishughulisha na uchimbaji wa dhahabu na wateja wengi wa bangi wanapatikana katika machimbo hayo.

Mtuhumiwa Masinde alipohojiwa, alikiri kulima zao hilo na kujitetea kuwa aliamua kufanya hivyo kutokana na kupata ushauri kutoka kwa kaka yake ambaye alikuwa akilima na masoko makubwa kupatikana katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wa Buswangili, Tambarare na eneo la Kalole.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Hamisi Misungwi, alisema wamejipanga kutokomeza ulimaji wa zao hilo kijijini hapo na kuongeza kuwa watawakagua wakulima kudhibiti kilimo hicho ambacho sasa wanahifadhi mpaka kwenye maghala.

Alisema walikagua katika shamba hilo na kubaini kuwa lina ukubwa wa hekari 10 na bangi nyingine ilikuwa imeshavunwa na kuhifadhiwa katika maghala hayo.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia tukio hilo akiwamo Ndebile Masanja, alisema wamesikitika kuona vijana wengi katika kijiji hicho wakiharibika.

Waliomba serikali kuweka mkazo kudhibiti kilimo zao hilo haramu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magirigimba, alitoa agizo kwa mtu aliyemwachia ofisi kufuatilia tukio hilo.

# BoT yakamilisha elimu usajili wa VICOBA

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imekamilisha utoaji wa elimu ya mfumo kwa maofisa ustawi wa jamii nchini kwa ajili ya usajili wa vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii (VICOBA).

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha, Victor Tarimu, alisema maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri mbalimbali wameshafundishwa namna ya kutumia mfumo.

"Tumeshatoa elimu mikoa yote na usajili wa VICOBA unaendelea, mifumo inafanya vizuri vikundi au wawakilishi wao wanapaswa kwenda halmashauri kukamilisha usajili," alisema.

Mwezi uliopita BoT ilifafanua kuwa katika usajili hakuna tozo, ada au kodi yoyote inayopaswa kulipwa na kikundi wakati wa usajili au wakati wakiendelea na shughuli zao.

Tarimu alisema mfumo wa usajili umekamilika na kila kikundi kinapaswa kusajiliwa na kwamba huchukua chini ya saa mbili kukamilisha na siku 14 halmashauri kutoa cheti cha usajili.

Kwa mujibu wa kanuni ya 4 hadi 7 mwaka 2019, watoa huduma ndogo za fedha (vikundi vya kijamii), kuwa ni kufanya mkutano wa awali, kamati ya mpito na majukumu yake na kikao cha uanzishaji na majukumu yake.

Mengine katika kanuni ya 8 hadi 17 ni maombi ya usajili yakiambatana na nakala ya katiba yenye sahihi za wanachama, nakala za mihtasari ya mkutano wa uanzishaji, maazimio ya wanachama kuanzisha kikundi.

Mengine ni mapendekezo ya muundo wa kikundi, uthibitisho wa malipo ya michango ya awali, barua ya mamlaka ya kata au kijiji, na jina la kikundi lijumuishe maneno 'kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii' na baada ya kukamilisha wanakikundi watatakiwa kufanya kikao cha kwanza ndani ya mwezi mmoja.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AccessBank Tanzania Limited** kupitia kampuni za madalali itauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Viwanja na Magari vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) tangu kutoka kwa tangazo hili, dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAMBA | BENARD /L. BENARD | SANGIJA/OREGA VERONICA | NYUMBA HATI NA. 52984 | LUCHELELE MWANZA | 01/04/2021 ALHAMISI SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2 | PAMBA | SHIJA /KIPEJA, LEONARD | SHIJA /KIPEJA, LEONARD | NYUMBA HATI NA. 53719 | IGOMA MWANZA | 02/04/2021 IJUMAA SAA 4:00 ASUBUHI |
| 3 | PAMBA | KYARUZI /G, GRATION | KYARUZI /G, GRATION | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE) | ILEMELA MWANZA | 03/04/2021 JUMAMOSI SAA 3: 00 ASUBUHI |
| 4 | PAMBA | MUSHI/ E. LAURENCE | MUSHI/ E. LAURENCE | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE | NYASAKA MWANZA | 05/04/2021 JUMATATU SAA 4:00 ASUBUHI |
| 5 | PAMBA | OMARY/ H. HASSAN | PETER/A, NDAKI | NYUMBA HATI NA. 20127 | NYAKATO MWANZA | 02/04/2021 IJUMAA SAA 4:00 ASUBUHI |
| 6 | PAMBA | RUTUNGO/ MUSSA. ADAM | RUTUNGO/MUSSA, ADAM | NYUMBA- HATI NA. 59002 | MUSOMA MJINI MARA | 03/04/2021 JUMAMOSI SAA 4:00 ASUBUHI |
| 7 | KAHAMA | MAKAKA/AMIN. NASIBU | MAKAKA/AMIN. NASIBU | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE) | KAHAMA MJINI SHINYANGA | 10/04/2021 JUMAMOSI SAA 3:00 ASUBUHI |
| 8 | PAMBA | BANDIO /L. GERMIN | BANDIO /L. GERMIN | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE) | MKOLANI MWANZA | 10/04/2021 JUMAMOSI SAA 4: 00 ASUBUHI |
| 9 | PAMBA | ESMAIL/IQBAL. MOHAMED | ESMAIL/IQBAL. MOHAMED | NYUMBA-HATI NA. 51785 | MKOLANI MWANZA | 09/04/2021 IJUMAA SAA 4:00 ASUBUHI |
| 10 | PAMBA | GRAYSON/W. MGIDANGE | GRAYSON/W. MGIDANGE | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE) | NYEGEZI MWANZA | 06/04/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |
| 11 | PAMBA | KATARAMA/SIMON.STRATON | SAMWEL/S, NEEMA | NYUMBA- HATI NA. 53947 | BWIRU MWANZA | 03/04/2021 JUMAMOSI SAA 4:00 ASUBUHI |
| 12 | PAMBA | DOMICIAN/ D. AUDAX | DOMICIAN/ D. AUDAX | NYUMBA- ALTERNATIVE MORTGAGE | NYASAKA MWANZA | 01/04/2021 ALHAMISI SAA 4:00 ASUBUHI |
| 13 | PAMBA | MGEMA/ O. PHILIPO | MGEMA/ O. PHILIPO | NYUMBA- ALTERNATIVE MORTGAGE | IGOMA MWANZA | 02/04/2021 IJUMAA SAA 4:00 ASUBUHI |
| 14 | MBEYA | MWAFUNGO/ANDREW,ASAJILE | MWAFUNGO/ANDREW,ASAJILE | ALTERNATIVE MORGAGE | MBEYA MJINI MBEYA | 30/3/2021 JUMANNE SAA 6:00 MCHANA |
| 15 | MBEYA | CHRISTOPHER,CLEMENT | CHRISTOPHER,CLEMENT | ALTERNATIVE MORTGAGE & HATI NA. 39421-MBYLR | MBALIZI MBEYA | 30/3/2021 JUMANNE SAA 6:00 MCHANA |
| 16 | MBEYA | PIPER FOODS &BEVERAGES | LUSWEMA/FELIX,PETER | NYUMBA | KYELA MBEYA | 29/03/2021 JUMATATU SAA 4:00 ASUBUHI |
| 17 | MBEYA | SUMUNI/MOHAMED,IDDI | SUMUNI/MOHAMED,IDDI | NYUMBA ALTERNATIVE MORTAGAGE | ISYESYE MBEYA | 30/03/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |
| 18 | MBEYA | MBAWA/ALTANAS, ISMAIL | MBAWA/ALTANAS, ISMAIL | NYUMBA GARI NAMBA T430 HYUNDAI SANTA | VETA MBEYA MJINI | 30/03/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |
| 19 | MBEYA | MLIMA MBEYA VIEW ACADEMY | MWAMFWAGASI/A,EPHRAHIM | SHULE, - HATI NA.4222-MBYLR. | NEW FOREST MBEYA MJINI | 30/03/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |
| 20 | MBEYA | SANGA/I, TUMAINI | TWEVE/L,HENRY | NYUMBA HATI NA. | MAFINGA IRINGA | 29/03/2021 JUMATATU |
| 21 | KIJITONYAMA | BOYSASA/KILEO, KIKI | AMINIEL RUMISHAEL URIO | PLOT NO. | UBUNGO KIBANGU DAR ES SALAAM | 30/03/2021 JUMANNE SAA 4: ASUBUHI |
| 22 | KIJITONYAMA | NGOTO/M.SOSPETER | NGOTO/M, SOSPETER | PLOT NO. 1794 BLOCK B, KINYEREZI ILALA | ILALA DAR ES SALAAM | 31/03/2021 JUMATANO SAA 4:00 ASUBUHI |
| 23 | KIJITONYAMA | MREMA/ ISSAYA HELGA | MREMA/ISSAYA, HELGA | NYUMBA-ALTERNATIVE MORTGAGE | UBUNGO DAR ES SALAAM | 29/03/2021 JUMATATU SAA 4:00 ASUBUHI |
| 24 | LUMUMBA | ISLAM/FESAL,SALHA | HUSSEIN/MHANDO, SAIDI<br>NGOPELA/HASHIM,MWANAHAMISI | NYUMBA- LESENI YA MAKAZI NA. TMK044855<br>NYUMBA LESENI YA MAKAZI NA.TMK044582 | MBAGALA KIBURUGWA TEMEKE DAR ES SALAAM<br>MBAGALA KWANYOKA TEMEKE DAR ES SALAAM | 01/04/2021 ALHAMISI SAA 4:00 ASUBUHI<br>29/03/2021 JUMATATU SAA 4:00 ASUBUHI |
| 25 | PAMBA | MARWA/E. JOSEPHAT | MARWA/E, JOSEPHAT | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 15623 | KISEKE MWANZA | 29/03/2021 JUMATATU SAA 4:00 ASUBUHI |
| 26 | PAMBA | SHIJA/PHILIP, SIMON | SHIJA/PHILIP, SIMON | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 65955 | NYASAKA MWANZA | 31/03/2021 JUMATANO SAA 4:00 ASUBUHI |
| 27 | TABORA | MALANGULA/KIPANGO, SHABANI | MALANGULA/KIPANGO, SHABANI | NYUMBA SHAHADA YA UMILIKI(ALTERNATIVE MORTGAGE) | TABORA | 30/03/2021 JUMANNE SAA 5:00 ASUBUHI |
| 28 | PAMBA | NCHEYE/R,DEO | MALUGU/M, PAULO | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 21536 | BUSWELU CENTRE ILEMELA MWANZA | 29/03/2021 JUMATATU SAA 8:00 MCHANA |
| 29 | PAMBA | MAKUNDI/R, FLORA | MAKUNDI/R, FLORA | NYUMBA | IGOMA MWANZA | 30/03/2021 JUMANNE SAA 3:00 ASUBUHI |
| 30 | LUMUMBA | MWAKISOLE/OBENI, MENGI | NJAWALE/COSMAS, MIRIAM | NYUMBA LESENI YA MAKAZI NA.TMK/MBK/MBK/25/177 | MBAGALA KUU TEMEKE DAR ES SALAAM | 30/3/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |
| 31 | LUMUMBA | NDAGHINE/RAMADHAN, ABDUL | KIRANGO/RASHID, MAIJA | NYUMBA LESENI YA MAKAZI NA. O42056 | AZIMIO, MTONGANI, TEMEKE DAR ES SALAAM | 31/3/2021 JUMANNE SAA 4:00 ASUBUHI |

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA KUSHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**ACCESSBANK TANZANIA LIMITED SIMU NAMBA. +255 677 860 000**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

# Mgomo daladala watikisa Mbeya, nauli hazishikiki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHUGHULI za usafiri na usafirishaji katika Jiji la Mbeya zimekwama baada ya madereva wa magari ya kusafirisha abiria maarufu daladala kugoma kufanya kazi wakishinikiza serikali kuziondoa bajaji kwenye barabara kuu.

Mgomo huo ulianza jana alfajiri ambapo madereva hao walisema bajaji zinasababisha kazi yao kuwa ngumu na kuwapunguzia kipato kutokana na kuingilia njia zao kwa kuchukua abiria kwenye vituo vilivyotengwa kwa ajili ya daladala.

Nipashe lilitembelea vituo mbalimbali vya daladala na kushuhudia idadi kubwa ya watu wakiwamo wanafunzi, wakiwa wanasubiri usafiri bila mafanikio, ambapo baadhi ya magari yalikuwa hayaonekani yalikohifadhiwa na baadhi yakiwa yameegeshwa kwenye vituo hivyo.

Hata hivyo madereva wa daladala hizo walikuwa wanazuia magari mengine yakiwamo yanayofanya safari zake kutoka katikati ya Jiji la Mbeya kwenda wilayani kubeba abiria, huku wakitaka bajaji pekee ndio ziachwe ziendelee kufanya kazi.

Baadhi ya wananchi walisema mgomo huo umeathiri shughuli zao zikiwamo za kiuchumi na kijamii kutokana na kuchelewa kwenda kwenye maeneo yao ya kazi.

Debora Njobel, mkazi wa Isanga jijini Mbeya, alisema alikuwa anaenda kazini kwake Uyole na alipofika katika Kituo cha daladala cha Kabwe saa 1:00 asubuhi alikuta hakuna magari kabisa.

Alisema usafiri pekee uliokuwapo ni wa bajaji ambazo hata hivyo zilikuwa zimepandisha nauli kutoka Sh. 400 ya kawaida mpaka kati ya Sh. 1,000 na 1,500 viwango ambavyo alisema vinawaumiza kutokana na uchumi wao.

"Tunapata shida sana maana huu mgomo umeanza ghafla sana na tunaumia maana nikilipa hii nauli ya Sh. 1000 mpaka Uyole natakiwa tena kutafuta usafiri mwingine kwenda kazini kwangu," alisema Debora.

Naye Angel Mbotwa aliiomba serikali kuziwekea bajaji na daladala utaratibu mzuri ili kuepusha mwingiliano kwenye njia ambao unasababisha migogoro ambayo inawaumiza wananchi wa kawaida.

Hata hivyo madereva wa daladala walisema waliamua kugoma kwa sababu bajaji zinawafanya wanashindwa kufanya kazi vizuri na kwamba kila wakiwaomba viongozi wa serikali wawasaidie huwa hawapati msaada.

Martin Mlay alisema walijibiwa na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, kuwa kama wamiliki wa daladala wanaona bajaji zinalipa zaidi wanatakiwa wauze daladala zao ili wanunuwe bajaji.

"Mkuu wa Mkoa alisema hayuko tayari kuziondoa bajaji barabara kuu na akasema tuuze daladala ili tununuwe bajaji, sasa mabosi wetu wameamua kuuza magari kama alivyosema Chalamila," alisema Mlay.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mgomo huo, RC Chalamila alisema hawezi kuziondoa bajaji kwenye barabara kuu kwa sababu ni miongoni mwa vyombo vinavyoajiri vijana wengi kwa sasa.

Alisema endapo madereva daladala hao wataendelea kugoma, atafuta vibali vyote vya magari hayo na kuamuru magari ya serikali yakiwamo ya vyombo vya dola kufanya kazi ya kusafirisha abiria.

"Mgomo sio njia sahihi ya kupata suluhisho la jambo lolote, naweza kufuta leseni zote na kuamuru mabasi ya Polisi, Magereza na hata ya mahakama kufanya kazi hiyo, na yeyote atakayetaka kurudi barabarani atatakiwa kwenda kuomba usajili mpya," alisema Chalamila.



Mkazi wa Panga la Muingereza, Kisarawe mkoani Pwani, Sabrina Iddy, akichota maji kwenye kisima jana, wakazi wa kijiji hicho wanatembea umbali mrefu kufuata maji kutokana na ukame wa mara kwa mara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kiwanga arejesha fomu uenyekiti BAWACHA

**Na Enock Charles**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambaye alikuwa Mbunge wa Mlimba kupitia chama hicho 2015-2020, Susan Kiwanga, jana alirejesha fomu ya kuwania nafasi ya Uenyekiti wa Baraza la Wanawake la chama hicho (BAWACHA), iliyoachwa wazi na Halima Mdee, aliyefukuzwa uanachama wa chama hicho.

Akizungumza baada ya kurejesha fomu hizo, Kiwanga, alisema lengo lake ni kupigania maslahi ya wanawake hasa kipindi hiki cha ugonjwa wa corona, wanawake ndiyo waathirika namba moja wa ugonjwa huo hatari, na kwamba akichaguliwa atakuja na mikakati ya kupambana na tatizo hilo.

"Mimi nimeguswa na baraza kutokuwa na uongozi na mambo mengi yanapita, lakini hakuna matamko yanayotolewa kwa kuwa kuna ombwe la uongozi," alisema.

Halima Mdee na wenzake 18 walitimuliwa uanachama na uongozi wa chama hicho mwaka jana, baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum, wakidaiwa kukiuka msimamo wa chama hicho.

**Mimi nimeguswa na baraza kutokuwa na uongozi na mambo mengi yanapita, lakini hakuna matamko yanayotolewa kwa kuwa kuna ombwe la uongozi.**

# Moto wateketeza mabweni shule ya sekondari

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MOTO mkubwa ambao chanzo chake bado hakijafahamika, umeteketeza jengo lenye vyumba vinne vilivyokuwa vikitumika kama mabweni ya wasichana katika Shule ya Sekondari Spring Valley Manispaa ya Iringa.

Imeelezwa wakati moto huo ukianza kuwaka, wanafunzi walikuwa madarasani wakiendelea na masomo ya jioni kabla ya kwenda kulala.

Akizungumza eneo la tukio kwa niaba ya Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Iringa, Koplo Abubakari Shindwa, alisema walipokea taarifa za tukio hilo majira ya saa 2 usiku na kukimbia kufika eneo la tukio kudhibiti moto huo, ambao tayari ulikuwa umeteketeza baadhi ya vyumba vya mabweni hayo.

"Baada ya kufika eneo la tukio tulifanikiwa kuuzima moto huu mkubwa japo kwa haraka haraka hatuwezi kujua thamani ya hasara iliyotokana na moto huo wala chanzo chake hadi hapo tutakapofanya tathmini na uchunguzi wa nini kilisababisha moto huo," alisema.

Alisema sababu kubwa ya moto huo kuteketeza sehemu kubwa ya majengo hayo ni ucheleweshaji wa taarifa, na iwapo taarifa ingefika kwa wakati, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuudhibitiwa na kuepusha madhara yaliyojitokeza.

Mmoja kati ya walimu wa shule hiyo ambaye hakupenda kutajwa jina lake kwa kuwa si msemaji, alisema mkuu wa shule hayupo shuleni hapo na kuwa moto huo umeleta madhara makubwa kwa wanafunzi ikiwamo mali zao kama vitanda, magodoro, nguo na vifaa vyao vingine kuteketea.

Alisema sehemu kubwa wanafunzi na walimu pamoja na wananchi wanaozunguka shule hiyo waliweza kufika kwa wakati na kufanikiwa kutoa baadhi ya vifaa vya wanafunzi hasa kwenye mabweni kama matatu hivi, ila sehemu kubwa moto umeweza kuteketeza mali zote za wanafunzi.

Kuhusu madhara kwa wanafunzi, alisema hakuna madhara ya mwanafunzi kuungua moto zaidi ya wanafunzi kadhaa kupoteza fahamu kutokana na mshtuko wa tukio hilo.

Jeshi la Polisi mkoani Iringa limethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwa linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo.

Kaimu Kamanda wa Polisi, Rienda Millanzi, alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walifika eneo la tukio kudhibiti moto huo na kufanikiwa.

# Aamuru m/kiti kuwekwa rumande hadi mtuhumiwa ubakaji apatikane

**Na Claudia Kayombo**

DIWANI wa Kata ya Chanika, Deogratius Masaburi, amemwagiza Kamanda wa Polisi Wilaya ya Kipolisi (OCD), Chanika, Joseph Mwakabonga, kumweka rumande Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ngwale wa kata hiyo, Bakari Matimbwa, mpaka mtuhumiwa wa kesi ya ukabaji, Abdul Upunda, atakapopatikana.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari, baada ya mkutano wa hadhara wa ulinzi na usalama ulioitishwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Vikongoro, Chanika, Seif Mwela.

Masaburi alisema ametoa amri hiyo akiunga mkono jitihada za serikali za kulinda na kudumisha amani ambavyo vinaanzia ngazi ya familia, mtaa hadi taifa, huku viongozi wakiwamo wenyeviti wa serikali za mitaa, wakiwa na wajibu wa kuisimamia.

Alifafanua kuwa hana ugomvi na mwenyekiti huyo ambaye upande mwingine anamwita baba kwa kuwa alimsaidia katika kampeni za kumweka madarakani, lakini katika suala la kutekeleza malengo ya serikali hana mchezo.

Alisema akiwa katika mkutano huo aliambiwa habari za vijana watatu ambao ni tishio la uvunjifu wa amani kwa kuwakaba wananchi, kuwapiga nondo na kuwanyang'anya mali zao na kwamba mmoja aliyekamatwa na kuwekwa rumande, alitolewa baada ya kuwekewa dhamana na mwenyekiti huyo na sasa ametoroka na hajulikani alipo.

Diwani Masaburi alisema anaamini kuwa kuwekwa rumande mwenyekiti huyo kutasababisha mtuhumiwa huyo kupatikana na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Awali, Mwenyekiti Mwera alimwomba OCD wa Chanika, kuwakamata vijana wawili ambao wanahatarisha usalama wa mtaa huo. Alisema kuwa anaamini kukamatwa kwao kutaondoa shaka waliyo nayo wananchi wa mtaa huo, kuhusu usalama wao na wa mali zao hususan wanapokatiza mtaani usiku na alfajiri.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo (wapili kulia), akiwaongoza wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo chini ya wizara hiyo, kula chakula kinacholiwa na wafungwa katika Gereza la Wilaya ya Singida, baada ya chakula hicho alipata fursa ya kuzungumza na wafungwa hao. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Shauri la kufutwa uwakili kwa mawakili 2 laahirishwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Maadili ya Mawakili imeahirisha kusikiliza kesi ya kufutwa uwakili inayowakabili mawakili Jebra Kambole na Edson Kilatu wanaotuhumiwa kuidharau Mahakama kinyume na maadili ya mawakili.

Kesi hiyo iliahirishwa jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam hadi Machi 19, mwaka huu, kutokana na akidi kutotimia.

Kesi hiyo ilifunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Oktoba 8, mwaka jana ambapo Wakili Jebra anatuhumiwa kuidharau mahakama kwa kuchapisha maudhui katika ukurasa wake wa Twitter kuwa "Kisutu Revenue Authority" kwa tafsiri isiyo rasmi ni "Mamlaka ya Mapato Kisutu".

Jebra anadaiwa kuchapisha maneno hayo baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwahukumu viongozi tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kulipa faini ya Sh. milioni 350.

Viongozi hao wa CHADEMA walikutwa na hatia ya makosa 12 ikiwamo kufanya maandamano yasiyokuwa na kibali, ambao walilipa faini hiyo na kutoka gerezani.

Kwa upande wake wakili Kilatu anatuhumiwa kwa kuchapisha maoni kwenye ukurasa wake wa Facebook Agosti 8, 2020, maoni ambayo ni ya kuikosoa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, lakini pia maoni ambayo yanaashiria kutoiheshimu Mahakama, sheria na taaluma ya sheria.

Maoni hayo pia yanadaiwa kuwa yanaashiria kuhamasisha umma usiwe na imani na mahakama. Kutokana na mawakili hao kwa nyakati tofauti kutoa maoni yao mtandaoni, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipeleka mashtaka kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili kuomba kamati itamke kuwa mawakili hao wamekiuka maadili ya taaluma ya sheria hivyo wafutiwe uwakili.

Septemba 20, mwaka 2019, Wakili wa kujitegemea Fatma Karume alisimamishwa kufanya kazi za uwakili Tanzania Bara baada ya kukutwa na hatia na kamati hiyo, kutokana na mwenendo wake kwenye mitandao ya kijamii.

Maamuzi hayo yalitolewa na Jaji Kiongozi, Eliezer Feleshi, kwenye kesi iliyofunguliwa na Katibu wa Uenezi wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, akipinga uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), ambayo wakili wake alikuwa Fatuma, ambaye alidaiwa kuandika kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na mwenendo wa kesi kwenye mitandao ya kijamii.

Karume amesimamishwa kazi huku sababu yake ikitajwa kuwa ni kile alichokizungumza katika kesi iliyofunguliwa na Shaibu kupinga uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Adelarus Kilangi, aliyeteuliwa na Rais John Magufuli, Februari Mosi, mwaka 2018.

# Ofisa ardhi kizimbani madai uhujumu uchumi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watatu wakiwamo mpima ardhi na mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Nahukukahuka, Halmashauri ya Mtama, Wilaya ya Lindi, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka sita likiwamo uhujumu uchumi la kujipatia fedha kinyume cha sheria.

Watuhumiwa hao ni Ofisa Ardhi Halmashauri ya Mtama, Mussa Mbinga, Mohamedi Mtungwe (Mjumbe Serikali ya Kijiji) na Hassani Mohamedi (mkulima), walifikishwa Mahakama ya Wilaya ya Lindi na kusomewa mashtaka yao na mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Osboru Mulamuzi.

Akiwasomea mashtaka yao mbele ya Hakimu Muyonga Makala, Mulamuzi alidai watuhumiwa wote kwa pamoja mwaka 2017, walijipatia kinyume cha sheria jumla ya Sh. 95, 562,449 kutoka kwa mwekezaji kampuni ya Cassava Starch of Tanzania Limited.

Mulamuzi alidai kuwa kiasi cha fedha wanazodaiwa kujipatia ni kati ya Sh. 450,336,500 zilizotolewa na kampuni hiyo kulipa fidia kwa wakulima wa Kijiji cha Nahukahuka kupisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza stachi inayotokana na zao la muhogo.

Kosa la pili ni kughushi nyaraka za serikali kinyume cha kifungu cha 332, 335 na 337 vinasomwa pamoja na kanuni ya adhabu sura ya 16/2019, na kosa la pili ni kutumia nyaraka kwa nia ya kumdanganya mwajiri kinyume na kifungu 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329/2019.

Makosa mengine ni kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na kifungu 302 cha Sheria Kanuni ya Adhabu sura 16/2019 na kosa lingine ni kuisababishia halmashauri hasara kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi sura ya 200/2019.

Hata hivyo washtakiwa hawakutakiwa kukubali wala kukataa, kwani kwa mujibu wa matakwa ya kisheria, mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za aina hiyo hadi Mahakama Kuu, shauri hilo la uhujumu uchumi namba 02/2012, limepangwa kutajwa tena Machi 26, mwaka huu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Urejeshaji mikopo elimu juu umulikwe kumkomboa maskini

**NI** ndoto ya watoto wengi wanaotoka katika familia zenye kipato kidogo, kufika chuo kikuu na kusoma kupitia mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na serikali.

Hata hivyo, shida inakuja pale vijana hao wanapohitimu masomo yao ya elimu ya juu na kutakiwa kuanza kurejesha mikopo waliyopewa.

Mwongozo wa utoaji mikopo hiyo inayosimamiwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), umeweka masharti kwamba mnufaika anapaswa kuanza kurejesha mkopo wake miaka miwili baada ya kuhitimu masomo yake, vinginevyo anapigwa penalti ya asilimia 10 ya mkopo huo.

Mwongozo huo pia umeweka masharti mengine ya deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka kuanzia tarehe ambayo mnufaika alianza kupata fedha. Hii ina maana kwamba, mnufaika aliyesoma chuo kikuu kwa miaka mitatu, kwa mfano, deni lake litakuwa limeongezeka kwa asilimia 18 ndani ya kipindi hicho cha masomo yake.

Katika mwongozo huo, yapo masharti ya kila mnufaika wa mikopo hiyo kutozwa asilimia moja ya mkopo wake kwa ajili ya uendeshaji wa bodi, jambo ambalo limekuwa likipingwa na baadhi ya wanufaika na wadau wa elimu nchini kwa mtazamo kwamba HESLB ni chombo cha serikali na watumishi wake wanalipwa mishahara na posho kama watumishi wengine wa umma, hivyo hakuna haja ya makato hayo kwa wanufaika wa mikopo ya bodi hiyo.

Nipashe tunaikumbusha serikali kufanyia kazi mapendekezo ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, ya Februari 11 mwaka huu kuhusu mikopo hiyo. Spika Ndugai aliungana na wabunge wengine siku hiyo kuitaka serikali ifanye mapitio katika urejeshaji wa mikopo hiyo, akionya kuwa sasa imegeuka biashara badala ya kumsaidia mtoto wa maskini.

Tunakumbuka pia wiki iliyopita, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizungumzia suala hili, ikisisitiza ipo mikakati inayoendelea kwa lengo la kufanyia kazi malalamiko kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo.

Mathalani, deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka kunalalamikiwa na wanufaika kutokana na kusababisha ugumu wa kumaliza kulilipa, japo bodi imekuwa ikitetea kwamba inafanya hivyo ili kulinda thamani ya fedha na kuufanya mfuko wake kuwa endelevu.

Takwimu zinaonyesha kwamba, hadi Agosti 2019, kati ya Watanzania 479,779 waliopewa mikopo hiyo tangu serikali ianze kuitoa mwaka 1994, ni 11,214 tu (sawa na asilimia 2.3) waliofanikiwa kumaliza kulipa deni lao. Sababu kubwa inayotajwa na wanufaika ni kitendo cha deni hilo kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.


Ni mtazamo wetu Nipashe kwamba ugumu uliopo katika kumaliza kulipa mikopo hiyo unazalisha vikwazo vingine vya kiuchumi kwa mtoto wa maskini aliyepata elimu ya juu kwa mkopo wa serikali, ikiwa ni pamoja na kushindwa kukopesheka kwenye taasisi zingine za kifedha.

Nipashe tunaviona vikwazo hivyo vya kiuchumi kwa kuzingatia sheria za nchi zinamtaka mnufaika kulipa deni hilo kwa kukatwa asilimia 15 ya mshahara wake (kama ni mwajiriwa) au kuilipa Sh. 100,000 kila mwezi kwa asiyeajiriwa, bila kusahau makato mengine yaliyopo kisheria ikiwamo michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, kodi ya serikali (PAYE), bima ya afya na vyama vya wafanyakazi.

Haya yote yanapunguza wigo wa mnufaika kukopeshwa kwenye taasisi za kifedha ikizingatiwa Benki Kuu (BoT) imeweka masharti ya makato kutozidi theluthi moja ya mashahara wa mwajiriwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuna wajibu wa kuwalinda na kuwatetea watoto wetu

Na Christina Mwakangale

**WATOTO** ni kundi ambalo ni maalumu kwenye jamii, linalotambuliwa na kulindwa na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Pamoja na sheria hiyo kuwapo, miongoni mwa jamii wanashindwa kutekeleza yaliyomo kwenye sheria iliyopo, ikiwamo kuwapa ulinzi na haki zao.

Hiyo inatokana na matukio kadhaa ndani ya jamii ambayo yanaripotiwa kwenye vyombo vya habari nchini, kuelezea matukio tofauti yanayowakumba watoto, baadhi wakifanyiwa ukatili wa kijinsia.

Mwanahabari mtangazaji nguli, Ahmed Kipozi, hivi karibuni akitoa uzoefu katika fani yake, anawakumbusha na kuwapa mbinu waandishi wa habari wa sasa, namna ya nguvu ya uandishi kuhusu matukio hayo na kuleta mabadiliko kwenye jamii.

Anasema ripoti moja kuhusu matukio hayo, inaweza kuibadili jamii na kuwafanya watoto waishi kwa amani kama wengine.

Kupitia uzoefu wake, anasema alijikita katika ripoti ambazo zinazogusia watoto na kuandaa hata miradi na kuwafikia kwenye maeneo tofauti, kuanzia miaka ya 1970 akiwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

"Katika habari hizi mwandishi usitake kujipatia umaarufu au kujenga jina hasa kuhusu namna unavyoripoti tukio, bali angalia kwanza ripoti yako imemsaidiaje mtoto ambaye ameathiriwa na tukio lolote la ukatili kama vile, kubakwa, kulawitiwa.

"Jaribu kuvaa viatu vya mtendewa kuhisi athari na maumivu aliyopitia mtoto huyo, kwanza amevunjiwa haki ya utoto wake, hajalindwa," anasema Kipozi.

Kipozi, aliyewahi pia kuwa Mkuu wa Wilaya Bagamoyo, ameyasema hayo hivi karibuni alipowasilisha mada kuhusu uandishi wa habari za watoto, kanuni na haki zao katika mafunzo ya siku mbili kwa wanahabari, jinsi ya kuripoti habari na kesi za watoto, yaliyoandaliwa na Asasi ya Child Rights Media Foundation (CRMF).

**Sheria hii pia imechukua mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa yanayohusu haki za mtoto, vilevile kutoka kwenye Sera ya Taifa ya Watoto.**

Kuhusu kanuni, Kipozi anasema kanuni za uandishi wa habari za aina hii ni pamoja na kulinda utu, haki, heshima kwa kila mtoto, bila ya kujali anatoka katika familia ya aina gani.

Anasema: "Kwa kuwa watoto wote ni sawa, hawana tofauti kwamba anayetoka kwenye familia ya tajiri ni bora zaidi kuliko wa maskini, hadhi zao kisheria zinafanana."

Pia anafafanua ulinzi wa mtoto ili asidhurike ni muhimu pale mwandishi anapoandika habari zake, kwa kulinda vyanzo vya habari ambavyo mtoto atavitaja pale anapohojiwa.

Anasisitiza mwandishi azingatie umri, kuhifadhi jina la mtoto, kumficha sura yake na pia uelewa wa mtoto na mtoto mwingine hutofautiana hivyo ahojiwe kulingana na sifa hizo.

Sheria ya Mtoto katika Sura ya 13 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019, ina vifungu ambavyo mtu anaweza kushtakiwa kwa kumfanyia mtoto ukatili.

Pia Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 ni waraka unaoshughulikia masuala mengi ya kitaifa yanayohusu haki na ulinzi wa mtoto. Sheria hii pia imechukua mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa yanayohusu haki za mtoto, vilevile kutoka kwenye Sera ya Taifa ya Watoto.

Ni sheria inayolenga kuimarisha ulinzi, matunzo na haki za watoto Tanzania Bara na imeainisha haki zake za kulelewa na wazazi, kupewa jina kuwa na utaifa, haki ya kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu, pamoja na haki ya kucheza na kuburudika.

Pia ni sheria inayoeleza wajibu wa mtoto pamoja na kufanya kazi kwa kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake watu wazima muda wote na atawasaidia pale inapohitajika.

HABARI KITAIFA

# Wajawazito Ushetu wakosa wodi yao

**Na Neema Sawaka,** USHETU

WAJAWAZITO katika kijiji cha Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, hawana huduma ya kujifungulia kutokana na zahanati ya kijiji hicho kukosa wodi na vitanda.

Hali hiyo huwalazimu wajawazito kwenda hospitali ya wilaya, mkoani Shinyanga kupata huduma.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ushetu, Dk. Mshahara Mpuya, alisema analazimika kuwapa rufani wajawazito kutokana na ukosefu wa wodi ya kujifungulia na vitanda.

Dk. Mpuya aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, wilayani humo.

Katika ziara hiyo kulikuwa na harambee maalumu na kupatikana Sh. milioni 6.8 na mifuko 160 ya saruji kwa ajili ya kujenga wodi ya wazazi.

Dk. Mpuya alisema wajawazito wakifika katika zahanati hiyo hupatiwa rufani kwenda kituo cha afya au hospitali ya wilaya kutokana na ukosefu wa chumba cha kujifungulia na wodi ya wazazi.

"Kipo chumba kimoja na kitanda kimoja wakifika wajawazito wawili wanataka kujifungua kwa wakati mmoja inakuwa ni shida, inanilazimu niwapatie rufani ya kwenda kituo cha afya kwani kwa mwezi wastani wa wajawazito 35 hadi 40 hujifungua hapo kwa shida," alisema Dk. Mpuya.

Mkuu wa Mkoa Telack, alisema fedha zitakazopatikana katika harambee hiyo, zitasaidia ujenzi wa wodi na chumba cha kujifungulia.

"Nimepata zaidi ya Sh. milioni 6.8 na mifuko ya saruji 160 nakukabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu ili ujenzi uanze mara moja kwani mama anapotaka kujifungua anahitaji faragha na hakuna haja ya rufani kama mama hana tatizo lolote," alisema Telack.

# Serikali kuwafutia leseni wachunaji ngozi Moro

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WIZARA ya Mifugo imesema itawachukulia hatua kali ikiwamo kuwafutia leseni wachunaji wa ngozi katika machinjio ya Manispaa ya Morogoro wanaotoboa ngozi za mifugo na kuikosesha thamani.

Akizungumza baada ya ziara ya kukagua uzalishaji wa ngozi bora zinazohitajika katika soko, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa mazao ya mifugo, usalama wa chakula na lishe, Gabriel Bura, alisema licha ya kufanyika mafunzo ya uchunaji bora wa ngozi, lakini kuna watu wanaokiuka taratibu.

Alisema mafunzo yaliyotolewa yamesaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa ngozi bora, na kwamba serikali haitawafumbia macho baadhi ya wachunaji wa ngozi wanaoendelea kutoboa ngozi kutokana na mahitaji makubwa katika viwanda vikubwa vya ngozi zilivyoanzisha.

"Tulizitoa leseni hizi kwa sheria ya ngozi namba 18 ya mwaka 2008, lakini tulitoa mafunzo ya uchunaji wa ngozi ili kuzipa thamani, baadhi yenu bado wanafanya makosa kwa kutoboa ngozi, sasa makosa haya yakijirudia tutawafutia leseni zao," alisema Bura.

Alisema serikali imejizatiti kwa kuanzisha na kufufua viwanda nchini ikiwamo kiwanda cha ngozi cha ACE Leather cha Morogoro na kiwanda cha ngozi cha Moshi na kuonya kitendo cha kuendelea kutoboa ngozi hizo ni kurudisha nyuma jitihada za serikali.

Aliwataka wachunaji hao kuendelea kuzingatia sheria katika utendaji wa kazi zao.

Joseph Kupa, Mkaguzi Mkuu wa nyama Manispaa ya Morogoro, alisema wanakabiliwa na changamoto ya baadhi ya watu kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na magonjwa ya ngozi.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni baadhi ya wafugaji kuendelea kupiga chapa mifugo yao jambo linalosababisha ngozi kukosa thamani huku magonjwa yakiendelea kushambulia mifugo.

"Changamoto tunazo pata mara nyingi ni mifugo inakuja hapa ikiwa imepigwa chapa na mingine imeshambuliwa na magonjwa ya ngozi sasa ikifika hapa inakuwa tayari haina thamani hata hatuwezi kuichuna kwa sababu haiwezi kununuliwa na inatokana na baadhi ya wafugaji kutokuwa na elimu ya kutosha ya umuhimu wa ngozi," alisema Kupa.

Mwenyekiti wa wachunaji wa ngozi, Mapinduzi Ernest, alishukuru kwa elimu waliyoipata ambayo inawasaidia kuzalisha ngozi bora na kuiomba serikali kufikisha elimu kwa wafugaji ya upigaji chapa ili kupata ngozi bora.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akizungumza wakati wa hafla ya kuwakaribisha waliokuwa wafanyakazi wa China Commercial Benki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi wa Benki ya China waripoti NMB

**Na Mwandisho Wetu**

BENKI ya NMB imetangaza kuwachukua rasmi wafanyakazi wote wa Benki ya Biashara ya China (CCB) ambayo umiliki wake ilikabidhiwa mwanzoni mwa mwezi huu na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Wafanyakazi hao 12 walipokelewa rasmi jana asubuhi makao makuu ya NMB jijini Dar es Salaam.

Matatizo ya mtaji na ukwasi yalipoanza na kufikia hatua ya CCB kuwekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu (BoT), wafanyakazi hao walikata tamaa, lakini taarifa za NMB kukubali kuzinusuru shughuli za mwajiri wao wa zamani ziliwapa matumaini makubwa ingawa hatima yao mwanzoni haikujulikana.

Furaha isiyo na kifani muda wote wa hafla ya kuwatambulisha jana ilikuwa ni ishara tosha ya utayari wao kumtumikia mwajiri wao mpya kwa bidii na kuwahudumia wateja wake zaidi ya milioni nne kwa nguvu na uwezo wao wote kama alivyosema mwakilishi wao, Phales Joseph Kiwanga.

Na hilo ndio NMB inalolitarajia na kutaka kutoka kwao kama ilivyoashiriwa na viongozi waandamizi wa benki hiyo ambayo imewaajiri kama hatua muhimu ya kimkakati ya kuziendeleza shughuli za CCB sokoni na kuwahudumia wateja na wadai wake wote kwa mtazamo tofauti kabisa unaolipa.

"Kwanza kabisa tulipata nguvu sana tuliposikia nia yenu ya kuichukua Benki ya Biashara ya China kwa sababu NMB ni benki kigogo inayoongoza kwa faida, mali, idadi ya wateja na upana wa kusambaza huduma zake sokoni," Kiwanga, alisema alipopewa nafasi ya kutoa neno kwa niaba ya wenzake.

"Pia tunatoa shukurani kwa uongozi wa NMB kwa kufanikisha zoezi la kuichukua CCB kwani kufanya hivyo kumetufungulia mlango mpya na mkubwa wa maendeleo ingawa mwazoni tulikosa kabisa usingizi kwa kutojua hatima ya ajira zetu lakini Mungu amesaidia NMB imetuchukua tunashukuru sana kwa hilo," aliongeza.

Uamuzi wa wa BoT kuimilikisha NMB shughuli za CCB ulitokana na kujiridhisha kuwa hiyo ndiyo njia muafaka ya kuzinusuru amana za wateja wake, kulinda maslahi ya wanaoidai na kuhakikisha uimara na uhimilivu wa sekta ya fedha kwa ujumla.

BoT ilipochukua uamuzi wa kuhamishia mali na madeni yote ya CCB kwenda NMB, na benki hiyo kubwa nchini kulikubali jukumu hilo, pia iliamua kuwachukua na wafanyakazi wote ili hasa waendelee kuwahudumia wateja wa mwajiri wao wa zamani.

"Leo ni siku ya furaha kwetu kama benki kwani tumeongeza ukubwa wa familia yetu kwa kuwapokea wenzetu kutoka benki ya kibiashara ya China nchini Tanzania. Nachukua nafasi hii kuwakaribisha sana NMB na kuanzia sasa, ninyi ni sehemu ya familia hii," Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna alisema.

# Waziri ashtuka fedha alizozitoa jimboni

**Happy Severine,** MASWA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Aswege Kaminyoge, kufuatilia matumizi ya fedha alizozitoa na michango ya wananchi kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Jimbo la Maswa Magharibi.

Waziri Ndaki ambaye ni Mbunge wa Maswa Magharibi, alitoa agizo hilo baada ya ziara yake ya siku mbili ya kutembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika jimbo hilo.

Alisema baadhi ya miradi ambayo ametembelea kuona utekelezaji wake hakuridhishwa na matumizi ya fedha alizotoa kiasi cha Sh. milioni 8 kwa ajili ya kuezeka jengo la zahanati katika Kijiji cha Funika katika Kata ya Isanga.

Waziri Mashimba alisema alitoa fedha hizo ili kununua mbao na bati kwa ajili ya kuuzeka jengo hilo ambalo limejengwa kwa nguvu za wananchi, lakini anashangaa kuona jengo hilo likiwa limeezekwa pungufu kwa mabati 24.

"Mkuu wa wilaya nakuagiza ufuatilie matumizi ya fedha hizo, ambazo nilitoa kwa ajili ya kuezeka jengo hili...haiwezekani nitoe fedha halafu zisitumike kama nilivyokusudia, maana nilitoa fedha za kununua mbao na mabati yote hizi zingine zimekwenda wapi?" Alihoji.

Awali Mtendaji wa Kijiji cha Funika, Jeremiah Misonga, akisoma taarifa za ujenzi wa zahanati hiyo alisema alipokea fedha hizo na walinunua mbao na mabati 168 na fedha ikawa imekwisha, lakini maelezo yake yalipingwa na Waziri Ndaki.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndaki alionyesha kutoridhishwa na ujenzi wa wodi ya wanawake wajawazito katika Zahanati ya Kijiji cha Isanga ambapo Mtendaji wa Kijiji hicho ambaye alitajwa kwa jina moja la Dionizi, alishindwa kutoa mchanganuo wa matumizi ya ujenzi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akikagua eneo la Mto Ruvu litakalotumika kama chanzo cha maji kwa shamba la Mkulazi lililoko Mkulazi, Morogoro Vijijini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Jafo aagiza benki zitoe huduma kidijitali

**Na Felix Andrew**

SERIKALI imeiagiza Benki ya Mwalimu Commercial (MCB) kuboresha jitihada za kuwafikia wateja wengi zaidi huduma za kidigitali.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, wakati akizindua huduma ya Mwalimucard Visa na huduma ya kidijitali jijini Dodoma.

"Haiwezekani mkashusha viwango hivyo vya gharama kwenda katika viwango shindani zaidi ambavyo kila mwalimu anakuwa na hamu ya kusema najiunga na kupata mkopo? Katika watu wanaopigwa vibaya sana ni walimu katika suala la mikopo," alisema.

Alisema wapo walimu wengine wamebambikiziwa mikopo yenye riba kubwa za ajabu na wapo wengine wanashindwa kuhudhuria vipindi na hivyo kufukuzwa kazi kwa sababu ya changamoto wanazopata kutokana na mikopo umiza.

Pia Waziri Jafo aliitaka benki hiyo kuwa na mkakati wa kuongeza idadi ya wateja kwa kuanzia kwa walimu nchini na watu wengine.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa bodi hiyo, Francis Ramadhani, alisema moja ya maeneo ya kipaumbele ya benki hiyo ni utoaji wa huduma za kibenki kwa njia za kidijitali na kuwafikia wateja wao.

Alisema benki hiyo imeanzisha huduma ya Banc assurance inawezesha wateja kukidhi mahitaji yao ya bima katika maisha yao ya kila siku ikiwa ni pamoja na kuwahikikishia usalama na fidia wakati wa majanga.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu (CWT), Deus Seif, aliwataka walimu wote kujiunga na benki ambayo itawawezesha kuchukua mikopo yenye riba nafuu.

Alisema ili kuondokana na wimbi la walimu wengi kuhudumiwa na kuchukua mikopo kwa watu wasiojulikana kupitia benki hiyo wataweza kukopeshana kwa riba zisizoumiza.

## Watakiwa kuchangamkia usajili majengo ya bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYABIASHARA wametakiwa kuchangamkia zoezi la utoaji elimu na usajili wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi, kwani hatua hiyo inalenga kuwatambua na kurahisisha utatuzi wa vikwazo vinavyowakabili.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkaguzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Alfred Kafaransa, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu ukaguzi unaoendelea kwenye majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi mkoani Pwani.

Kwa mujibu wa Kafaransa, usajili na elimu hiyo inayotolewa mlango kwa mlango unahusisha majengo yote yanayohusika na uuzaji wa chakula, ikiwamo baa, hoteli na mighahawa.

Alitaja maeneo mengine ni maduka yanayouza vyakula na vipodozi ya jumla na rejareja na sehemu zote zinazohusika na utunzaji vyakula kama maghala na mashine za kusaka na kukoboa vyakula.

Alisema usajili huo unaenda sambamba na kuwatambua wafanyabiashara wote.

"Tukishawatambua tunawaingiza kwenye mfumo na inakuwa rahisi kuwasaidia kama kuna changamoto zozote zinazowakabili, kwani tutakuwa na kanzidata yao na mawasiliano, hivyo tunaweza kuwasiliana nao wakati wowote na wao inakuwa ni rahisi kupata huduma kutoka kwetu," alisema Kafaransa.

Alifafanua kuwa lengo kuu ni kupita kwa wafanyabiashara ambao walikuwa hawajasajiliwa kujitokeza kujisajili kwenye mfumo wa shirika hilo na kuwa zoezi hilo ni rafiki.

"Kwa hiyo wale wote waliokuwa wakipata changamoto yoyote ya kuingia kwenye mfumo, tunawaelekeza cha kufanya ikiwa ni pamoja na kuwafungulia akaunti zao za barua pepe kwa wale ambao hawana ili wazitumie kujisajili kwenye mfumo," alisema.

Alisema katika Mkoa wa Pwani walianzia Mkuranga Mjini, Vikindu, Kisemvule, Mwandege, Kongowe hadi Kimanzichana Kusini.

Alisema baada ya kumaliza Mkuranga walihamia wilayani Kisarawe, ambapo walifanyakazi hiyo makao makuu ya Kisarawe, Kiruvya A na B na kisha kumalizia kazi yao Makuranga.

Alisema mpango huo ni endelevu kwa hiyo baada ya wao kumaliza timu awamu ya kwanza timu nyingine ya wakaguzi wa TBS itaenda mkoani Pwani kumalizia maeneo ambayo hawakuyafikia.

Alisema utaratibu huo ulikuwapo, kwani kabla ya hapo kazi hiyo ilikuwa inafanya na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) na kwamba baada ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019, jukumu hilo lilihamishiwa TBS.

# Dar kusambaza dawa folic acid vituo vya afya

**Na Sabato Kasika**

MKOA wa Dar es Salaam unatarajia kusambaza dawa za folic acid kwenye vituo vyote vya afya kusaidia kukabiliana na tatizo la kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu wa Afya wa mkoa huo, Sister Mathew, wakati akifungua semina ya mafunzo kwa wanahabari kuhusu umuhimu wa kuandika habari za kuelimisha umma kuzingatia suala la lishe bora.Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa, Mathew, alisema ofisi yake inajipanga kuhakikisha kila kituo cha afya mkoani humo kinakuwa na dawa za kutosha za folic acid.

Semina hiyo iliandaliwa na Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT), Asasi ya Child Help Tanzania na Chama cha Wazazi wa Watu Wenye Ulemavu wa Kichwa kikubwa na Mgongo Wazi Zanzibar.

"Tutahakikisha vituo vyote vya afya mkoani kwetu vinakuwa na dawa hizo ambazo ni za muhimu kusaidia kupunguza tatizo la wazazi kuzaa watoto wenye vichwa na mgongo wazi," alisema Mathew.

Alisema, pamoja na kusambaza dawa hizo, ipo haja ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuachana na mila potofu kuhusu uwapo wa tatizo hilo la kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

"Kumekuwapo na imani potofu na unyanyapaa, hivyo ni muhimu elimu itolewe kwa wingi ili jamii iwe na uelewa na kula lishe bora na vidonge vya madini ya chuma," alisema.

Ofisa Mawasiliano wa Taasisi ya Child Help Tanzania, ambaye ni Katibu wa ASBAHT Mkoa wa Dar es Salaam, Milton Byemerwa, alisema, ipo haja kuvijengea uwezo vyombo vya habari ili kupambana na ugonjwa huo.

"Vyombo vya habari vina nafasi nzuri ya kuhamasisha masuala muhimu ya kijamii na kiuchumi, hasa lishe bora na namna ya kukabiliana na utapiamlo, udumavu ili kupunguza, kama sio kuondoa kabisa tatizo la uzazi wa watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi," alisema Byemerwa.

Aliwaomba wanahabari kutumia kalamu zao kuhamasisha lishe bora hasa matumizi ya vyakula vyenye wingi wa vitamini ya foliki asidi ambavyo vinapatikana katika maeneo mengi yanayoizunguka jamii.

Meneja mradi wa programu za uongezaji virutubishi katika vyakula kutoka taasisi ya kimataifa ya Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Archard Ngemela, alisema virutubishi katika vyakula ni vya muhimu.

"Hayo yote ikiwamo utapiamlo yanatokana na upungufu wa virutubishi mbalimbali, hivyo ni muhimu kula vyakula vyenye virutubishi, kwani hata mafuta ya kula, unga mahindi vimeongezwa virutubishi," alisema Ngemela.

Alisema, chakula ambacho binadamu anakula, ndicho kinachoupatia mwili virutubishi au vitu vinavyotoa nguvu mwilini, kuusaidia kukua, kupambana na maradhi na kwamba suala la virutubishi ni la muhimu.

# JKT Mafinga kuongeza uzalishaji maziwa

**Na Renatha Msungu,** MAFINGA

KIKOSI cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mafinga mkoani Iringa, kinatarajia kuongeza idadi ya lita za uzalishaji maziwa kutoka 250 hadi 1,000 kwa siku ili kukikidhi mahitaji ya vikosi vya jeshi hilo, ikiwamo kuuza katika soko la ndani.

Aidha, jeshi hilo limejipanga kuongeza idadi ya ng'ombe wa nyama na maziwa inaofuga katika kambi ya JKT Mafinga lengo ikiwa ni kutekeleza agizo la Mkuu wa Jeshi hilo la kuwataka kujitegemea katika mhitaji ya chakula badala ya kusubiri fedha za serikali.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Kamanda wa Kikosi 841 Mafinga JKT, Luteni Kanali Issa Chalamila, wakati wa ziara ya waandishi wa habari waliotembelea kambi ya kikosi hicho, iliojikita katika ufugaji wa mifugo mbalimbali pamoja na kilimo.

Luteni Kanali Chalamila alisema hivi sasa kikosi hicho kinazalisha lita zaidi ya 200 za maziwa kwa siku, lakini katika mikakati walioiweka wamepanga kufikia kuzalisha lita 1,000 kwa siku ambazo zitakuwa zikitumika na ndani ya vikosi vya jeshi hilo, pamoja na kuwauzia jamii inayowazunguka.

"Moja ya mikakati tulijiwekea ni kuhakikisha tunafikia uzalishaji wa lita hizo kwa siku, kwa sababu tunaiboresha mifugo yetu kwa kushirikiana na wataalamu wa mifugo tulionao hapa kikosini," alisema.

Alisema kikosini hapo wana ng'ombe aina ya chotara na kienyeji ambao wote huboreshwa kupitia wataalamu jambo ambalo huchangia kwa kiasi kikubwa mifugo hiyo kutoa kiasi kingi cha maziwa kwa siku.

Hata hivyo alisema ukiacha ng'ombe wanaofugwa ndani ya kikosi hicho, pia wanafuga mbuzi, kondoo ambao nao ni sehemu ya mifugo iliopo kwenye mikakati ya kuboreshwa kuhakikisha inatoa mazao yaliyo bora.



Diwani wa Viti Maalum wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Diana James (wapili kushoto), akimkabidhi Justa Nzinza baiskeli kwa ajili ya mtoto wake mwenye ulemavu jana katika Kijiji cha Nyaseke, Kata ya Bulela, mkoani Geita. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Mkumbo aitaka TADB kutoa mafunzo ya maandiko miradi

**Na Mwandishi Wetu,** MPANDA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, ameiomba Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kutoa mafunzo ya maandiko ya miradi kwa watu wenye kutaka kuwekeza ili wapate mikopo na kuchochea uwekezaji katika sekta za kilimo na viwanda.

Prof. Mkumbo alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa wa Katavi hivi karibuni.Waziri alisema kuwa TADB ikitoa elimu hiyo, itakuwa ikishiriki kitaalamu katika kuchochea uwekezaji katika sekta hizo mbili.

"TADB ina nafasi kubwa ya kuongeza uwekezaji wa viwanda vinavyochakata mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo na moja ya njia nzuri ya kuongeza uwekezaji huo ni kutoa elimu ya uaandaji wa maandiko ya miradi," alisema Prof. Mkumbo.Alisema wawekezaji na wakulima watapata mikopo kutoka TADB na taasisi nyingine za kifedha iwapo watapata mwongozo wa uandaaji bora wa miradi na kwamba wanufaika wakipata fedha na kuwekeza taifa litanufaika.

"Tupo katika kutekeleza azma ya kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025, hivyo tufikirie uwezeshaji kwa njia ya mafunzo na mitaji kuwa ni vitu muhimu kwa taifa kufikia malengo yake," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema kuwa upatikanaji wa fedha unategemea namna andiko la mradi lilivyoandaliwa na kuongeza kwamba andiko budi liwe na ushawishi kwa taasisi za kifedha na taasisi zione haja ya kutoa mikopo kwa waombaji.Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema wamepokea mapendekezo ya waziri na kuahidi kwamba watayafanyia kazi ili miradi katika sekta ya kilimo ipate fedha na zitumike kuendeleza sekta za kilimo na viwanda nchini.

# Diwani amsaidia baiskeli mtoto mwenye ulemavu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

DIWANI wa Viti Maalum wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Diana James, ametoa msaada wa baiskeli kwa mtoto mlemavu mwenye umri wa miaka 5 ambaye anasoma chekechea katika Shule ya Msingi Igwata Kijiji cha Nyaseke Kata ya Bulela mkoani Geita.James alisema baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuwa kuna mama mmoja ana mtoto mwenye ulemavu, kila siku asubuhi huwa anambeba mtoto wake na kumpeleka shule, alikwenda shuleni kuhakikisha kama kweli mtoto huyo yupo.

Alisema alipofika shuleni hapo alijionea mwenyewe jinsi mama huyo alivyokuwa akimbeba shingoni na mgongoni akiwa amembeba mtoto mwingine, hivyo alimwonea huruma na kuamua kumnunulia baiskeli, aqmbayo hata hivyo hakutaja gharama zake.Kwa upande wake, mama huyo, Justa Nzinza, alimshukuru diwani huyo kwa msaada huo, na kueleza kuwa alimzaa mtoto wake huyo Kulwa Msole mwaka 2017 akiwa na pacha wake Doto Msole, ambaye alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 3 na baada ya mtoto huyo kupata ulemavu wa miguu yote na baba yao alikimbia na kumuacha akiwa na watoto tisa.

# Madiwani wakosoa takwimu za Ukimwi

Na Dinna Maningo, TARIME

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, mkoani Mara wametaka kuwekwa wazi takwimu za watu waliopima maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwenye taarifa zao ili kuwawezesha kujadili suala hilo.

Walisema takwimu za Ukimwi zinapowekwa wazi zinasaidia kufahamu ni maeneo gani yenye maambukizi mengi na maeneo ambayo maambukizi yapo chini ili kuwawezesha wadau mbalimbali kutoa elimu ya kujikinga kwa wananchi.

Madiwani waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati mwenyekiti wa kamati ya Ukimwi ambaye ni makamu mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Victoria Mapesa, akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Ukimwi (CMAC) ya robo ya pili 2020/2021.

Madiwani walikosoa taarifa hiyo kutokana na kutokuwa na takwimu za Ukimwi.

Mapesa alisema shughuli zilizofanyika ni pamoja na maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kwa utoaji wa huduma za upimaji VVU, tohara kwa wanaume, uchunguzi wa saratani ya kizazi, uchangiaji damu na huduma za macho.

Akizungumzia suala la utoaji wa mipira ya kiume (kondomu), alisema kuwa, Shirika la PSI lilitoa kondomu 37,152.

"Taarifa ya Ukimwi kutoka Idara ya Afya inahusu huduma ya upimaji wa VVU kwa kila vituo, hali ya upimaji kati ya wanaume na wanawake, huduma ya upimaji VVU kwa watoto chini ya miaka 14, hali ya magonjwa ya ngono, huduma za upimaji kwa wajawazito na huduma za wateja wanaotumia dawa za ARVs," alisema.

Baada ya taarifa hiyo Diwani wa Kwihancha, Ragita Mato, aliikosoa taarifa hiyo kwa kutoonyesha takwimu za upimaji wa VVU kwa wanaume, wanawake, wajawazito na watoto takwimu za magonjwa ya ngono na wagonjwa wanaotumia dawa za ARVs.

"Ni vizuri tujue takwimu za hali ya maambukizi ya VVU magonjwa ya ngono kwa nini hamjaziandika? ni lazima tujue kama maambukizi ni mengi au yameshuka, tujue waliopima VVU walikuwa wangapi kati ya hao waliokutwa na maambukizi ni wangapi ambao hawana ni wangapi, hivyo hivyo kwa wajawazito, watoto, wanaume kwa wanawake na tujue wangapi wamejiunga kutumia dawa na ambao hawatumii dawa za ARVs.

"Hali ya maambukizi ya magonjwa ya zinaa hatujui wangapi wamepimwa walikuwa na magonjwa yapi je, ni kaswende au kisonono, lakini taarifa haionyeshi, zaidi tu ya kutuambia tu upimaji usiokuwa na takwimu sasa tutajadili nini kama hakuna takwimu ambazo ndiyo zingetuwezesha kujadili kujua hali ya maambukizi ikoje ili tutafute ufumbuzi wa tatizo," alisema Mato.

Diwani wa Gwitiryo, Nashon Mchuma, alisema walishafanya vikao na walifuatilia kisha kuambiwa hawapaswi kuonyesha takwimu kwamba zinabaki kuwa siri.

"Hatuhitaji majina yao sisi tunataka kujua takwimu yaani takwimu zinakuwaje siri. Madiwani tutaelewaje hali ya kuenea kwa VVU bila kuwa na takwimu zake ambazo zitakupa dira uanzie wapi uishie wapi, unatoa elimu kwa wananchi kwamba tujihadhari na ukimwi ni hatari unaua wanakuuliza ni hatari kwa kiasi gani au umepungua kwa kiasi gani utawajibu nini?" Alisema.

Diwani wa Viti maalumu, Mariam Mkono, alisema takwimu za Ukimwi ni lazima wazifahamu kwa kuwa ndiyo wenye wananchi, lakini alisisitiza elimu ya Ukimwi iendelee kutolewa kwa kuwa kwa sasa kumekuwa kimya na watu wanadhani Ukimwi haupo hali ambayo inaweza kusababisha kuongezeka kwa maambukizi ya VVU.



Mkazi wa Pugu jijini Dar es Salaam, akiokota mkaa katika kituo cha mabasi ya Kisarawe Mkoa wa Pwani jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima wa chai kunufaika na mikopo

Na Mwandishi Wetu, NJOMBE

WAKULIMA wa chai wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuchukua na kunufaika na mikopo inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwani mikopo ni kati ya fursa zinazotolewa na benki hiyo.

Hayo yalibainishwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wiki iliyopita alipokuwa akishiriki katika mkutano wa wadau wa zao la chai unaoendelea hapa, ambapo pia alipongeza benki hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali zinazochangia kuinua sekta ya kilimo.

Mkutano huo ulijumuisha wakulima, wenye viwanda vinavyochakata chai na unajadili namna ya kutatua changamoto, na kuongeza tija za uzalishaji wa zao la chai kwenye ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Alitoa wito kwa wakulima wa chai kuchangamkia mikopo ya riba nafuu inayotolewa na TADB ili wapate matrekta na pembejeo nyingine ili wajikomboe kiuchumi.

"Nataka ni wahakikishie kwamba mkakati wa serikali ni kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo zote, mbegu, dawa, mbolea na vitendea kazi vinapatikana ili kumwezesha mkulima kufanya kazi yake kwa urahisi zaidi na ndiyo maana benki leo zinatoa fursa kwa mtu mmoja mmoja au ushirika kukopa matrekta na vyombo vingine vitakavyowasaidia kuendesha shughuli za kilimo," amesema Majaliwa.

Ofisa Kilimo wa Benki ya TADB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ashura Akimu, alisema benki yao itafanya kila liwezekanalo kutatua changamoto za wakulima wadogo, wakati na wakubwa.

Ametoa mfano wa usafirishaji wa chai na kusema kwa kuwa serikali itajenga barabara, benki itatoa mikopo kwa wakulima ili chai yao ifikike kiwandani kabla ya saa sita kuisha.

# Wakurugenzi waagizwa usimamizi miradi maji

Na Said Hamdani, LINDI

SERIKALI mkoani Lindi, imewaagiza wakurugenzi watendaji wa Halmashauri, Manispaa na Miji midogo kuwaelekeza watendaji wa kata kuhakikisha wanasimamia kikamilifu miradi ya maji na vyanzo vyake katika maeneo yao.

Lengo ni kila jamii iweze kunufaika na upatikanaji wa huduma hiyo muhimu.

Agizo hilo lilitolewa na Kaimu Mkuu wa Mkoa huo, Shaibu Ndemanga, wakati anafungua kikao cha wadau wa sekta ya maji, mkoa, na kwamba serikali imedhamiria kupambana kuhakikisha wananchi wanaondokana na adha ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Aliwataka watumishi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Mijini na Vijijini watekeleze majukumu yao.

# Red Cross yawapa taulo wanafunzi wa kike

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

CHAMA cha Msalaba Mwekundu (Red Cross) mkoani Shinyanga, kimetoa msaada wa vifaa vya shule na taulo za kike kwa wanafunzi 8,170, ambao wanaishi katika mazingira magumu wanaosoma shule za msingi Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Imeelezwa kwamba lengo, ili kuwajengea mazingira rafiki ya kusoma.

Meneja mradi wa chama hicho mkoani Shinyanga, Dismas Kiwale, alisema juzi kuwa wametoa msaada wa vifaa hivyo, ili kuwapunguzia vikwazo vya elimu wanafunzi ambao wanaishi katika mazingira magumu.

Alisema taulo hizo zitawasaidia kuhudhuria masomo kipindi wanapokuwa kwenye hedhi.

Aidha, alisema vifaa vya shule walivyotoa yakiwamo madaftari, kalamu, viatu, begi, sare za shule na taulo za kike, vitawasaidia wanafunzi hao kupunguza vikwazo katika masomo yao, na hatimaye kuwa na hali ya kupenda shule na kufanya vizuri kwenye mitihani yao. "Tumetoa msaada huu kwa ambao wanaishi katika mazingira magumu pamoja na wanafunzi wa kike tumewapatia taulo za kike kwa ajili ya kujistiri na hedhi kipindi cha masomo," alisema Kiwale.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema vifaa hivyo vitawasaidia watoto hao kupenda elimu pamoja na wanafunzi wa kike kutokosa vipindi vya masomo darasani wanapokuwa katika hedhi, na hatimaye kufanya vizuri kwenye masomo sawa na wavulana.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 16, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

Shule za Kigoma katika janga la 'kumi bora' kuanzia mkiani



Ukurasa 13

Mtandao jamii, kirusi kitafunacho kizazi kilichopo kwa kasi ya kutisha



Ukurasa 14

## Mchungaji aandika kitabu chenye somo kamili linalofanikisha ndoa

REO NA KILIO CHA MKOA LINDI...

**NA SABATO KASIKA**

# Licha kung'ara mtihani kitaifa, utoro kidato cha kwanza tatizo

UHABA wa madarasa ni mojawapo ya matatizo ambayo yamekuwa yakizikabili shule mbalimbali za sekondari nchini, ilhali kila mwaka kusababisha baadhi ya wanafunzi kutoanza masomo kwa wakati.

Badala yake wanaendelea kupangiwa shule kadri mikoa na halmashauri zinavyokamilisha ujenzi wa madarasa, pia watendaji wa sekta ya elimu katika ngazi zote wakiagizwa kuongeza bidii za usimamizi na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu, ili kufikia malengo ya elimu yaliyopangwa na serikali.

Wakati hilo limezoeleka la uhaba wa madarasa kila mwaka, kuna linalohusu utoro wa wanafunzi kwenye baadhi ya mikoa, hali inayochangia kukwamisha maendeleo ya elimu ya mwanafunzi.

Hivi katibuni Nipashe iliripoti wanafunzi 2,162 sawa na asilimia 13 kati ya 15,860 waliochaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari mkoani Lindi mwaka huu, hawajaripoti katika shule walizopangiwa.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Lindi, Vicent Kayombo ana ufafanuzi kuhusiana na hilo, anasema hoja kuu ya kuwapo walakini huo, ni wanafunzi kuwa watoro, kwani hadi Februari 26, mwaka huu, wanafunzi ambao hawakuripoti shule walizopangiwa ni wasichana 1,157 na wavulana 1,005, jumla yao 2162.

Kayombo anatoa mgawanyiko kiwilaya, Halmashauri za Nachingwea na Kilwa zikiongoza kwa idadi kubwa, akiwa na ufafanuzi: "Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina wanafunzi wasioripoti 481; Nachingwea 452; Mtama 390; Ruangwa 353; Liwale 292 na Lindi Manispaa 194."

Kutokana na utoro huo, anasema baadhi ya wazazi na walezi wameanza kuchukuliwa hatua ambazo hata hivyo, hakuziweka wazi, lakini zinalenga kuhakikisha wanafunzi wanahudhuria masomo shuleni.

Pia anasema kuna baadhi ya wazazi wameamua kuhamisha watoto wao na kuwapeleka shule nyingine binafsi, pasipo mawasiliano na mamlaka inayowafanya waonekane watoro.

Pia Ofisa Elimu huyo anasema kuna shaka kwa baadhi ya mabinti walioozeshwa na kuwapo watoto wasio na mwamko na kuamua kukaa nyumbani, kwa kukosa utashi wa kuendelea na masomo.



Wanafunzi katika shule mojawapo ya sekondari iliyoko wilayani Kilwa, mkoani Lindi, ilipokabiliwa na uhaba wa madawati. **PICHA: MTANDAO**

### SHEREHE YA KUJIPONGEZA

Wiki iliyopita, mkoa wa Lindi ulifanya sherehe za kujipongeza kwa kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa ya shule za msingi na sekondari na kutoa vyeti na tuzo mbalimbali kwa wilaya za mkoa huo.

Ni sherehe zilizofanyika wilayani Nachingwea na kuhudhuriwa na wakuu wa wilaya, maofisa elimu na wadau wengine wa elimu wa wilaya hizo, huku mgeni rasmi akiwa Katibu Tawala wa Mkoa Lindi, Rehema Madenge.

Mbali na kutolewa vyeti na tuzo mbalimbali, sherehe hizo, zilizinduliwa na Mpango wa Ufuatiliaji Elimu wa Pamoja. Pia ilizinduliwa mikakati ya kusimamia elimu ya mwaka 2021/2022.

Katibu Tawala anawataka wadau wa elimu kuendelea kutoa ushirikiano, katika kuinua kiwango cha elimu, ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa mazingira na miundombinu ya shule.

Anasema mikakati hiyo ni pamoja na upatikanaji wa chakula shuleni kama chachu ya ufaulu, kwamba ni suala muhimu kwa wadau wote na hasa wazazi na walezi kushiriki kikamilifu kwa maendeleo ya kielimu ya watoto wao na likasimamiwa kikamilifu na kufuatiliwa.

Rehema anataja haja ya kuwapo vita thabiti kukabili utoro kwa shule za Lindi, kukomesha mimba za wasichana shuleni na umuhimu wakusimamia utoaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

Walimu kwa upande wanaelekezwa haja ya kukamilisha mada zao mapema, kusimamia na kuendesha vituo vya mada ngumu, usimamizi na ufuatiliaji wa ujifunzaji shuleni.

Katibu Tawala huyo anawataka wadau wote wa Lindi kushirikiana katika kuhakikisha mpango mikakati hiyo inatekelezwa kikamilifu kwa kila mmoja kufanya ufuatiliaji kwenye eneo lake, ili kuendelea kuuweka mkoa huo juu kielimu.

ELIMU

NA PENDO THOMAS,
KIGOMA

# Shule za Kigoma katika janga la 'kumi bora' kuanzia mkiani

• Miaka 3 mfululizo hakuna mabadiliko • Walimu wafunguka siri, REO ajipanga



Wanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mgumile, Kata ya Kagera, Manispaa ya Kigoma Ujiji, wakiwa katika madarasa ya muda, baada ya shule yao kuzingirwa na maji kutoka Ziwa Tanganyika. **PICHA: PENDO THOMAS**

UKIUTAJA Mkoa wa Kigoma, basi wazo linaangukia zao la chikichi, linalotumika kuzalisha mafuta ya mawese.

Hata hivyo, katika maendeleo bado Kigoma inakabiliwa na shida kubwa ya ngazi ya ufaulu ngazi ya shule za msingi, jambo linaloibua maswali mengi kuhusu mstakabali wa elimu ya watoto wa mkoa huo.

Katika matokeo ya darasa la saba umekuwa siyo wa kuridhisha, ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara zikiwamo majirani Geita, Mwanza na Kagera.

Ikirejewa matokeo ya mtihani wa darasa saba unaofanyika kila mwaka na kutangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania (NECTA), sasa ni miaka mitatu mfululizo tangu 2017, kitaifa Kigoma inaogelea katika mikoa 10 ya mwisho.

Kwa mujibu wa matokeo yanayotangazwa na NECTA, kati ya mwaka 2017 na 2019, Kigoma haijawahi kutoka kwenye orodha ya mikoa 10 inayofanya vibaya kitaifa katika ngazi hiyo ya elimu.

Ni hali inayotawala, huku mtihani wa darasa la saba ukiwa ni daraja muhimu kumwezesha mwanafunzi kujiunga na shule za sekondari na panapo ufaulu, wanafikia vyuoni.

> "Hata hivyo, katika matokeo ya mwaka jana, NECTA haikufanikiwa kutoa mpangilio wa ufaulu kimkoa.

Takwimu za mpangilio wa mikoa kwa ubora wa ufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) uliotolewa na NECTA, zinaonyesha kuwa mkoa huo ulishika nafasi ya 21 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara katika mtihani wa mwaka 2019.

Takwimu zinaonyesha, Kigoma iliyoko Magharibi mwa nchi na imepakana na nchi ya Burundi, ilipata ufaulu wa asilimia 75.5 ukiwa chini ya wastani wa kitaifa wa asilimia 84.7 kwa mwaka huo.

Katika orodha hiyo ya 2019, mikoa iliyofanya vibaya, pia imo Manyara, Tabora, Dodoma, Singida, Songwe, Tanga, Lindi, Shinyanga na Mara iliyoshika nafasi ya mwisho kitaifa kwa wastani wa ufaulu wa asilimia 69.7.

Licha ya matokeo hayo duni, Kigoma mwaka juzi haikuingiza shule wala halmashauri moja katika orodha ya shule, halmashauri zilizofanya vibaya kitaifa.

**ILIKUWA BAHATI MBAYA?**

Kiwango duni cha ufaulu iliyopata mwaka 2019, ina sura ya kutokuwa bahati mbaya, kwa sababu miaka miwili kabla iliendelea kung'ang'ania katika orodha ya mikoa 10 mkiani kitaifa.

Mwaka 2017, Kigoma ilishika nafasi ya 18 kitaifa kati ya mikoa 26 kwa kupata wastani wa ufaulu wa asilimia 67.52. Hapo ndipo, ikaanza simulizi za 'mzimu' wa nafasi 10 mkiani ulipoanza kuushikilia mkoa. Kisha, mwaka uliofuata 2018, mkoa ulishuka zaidi hadi nafasi ya 25 kitaifa, ambayo ni ya mwisho kasoro moja, ilipokuwa na wastani wa ufaulu wa asilimia 67.65, kuutangulia mkoa wa Mara, ulioshikilia mkia kitaifa.

Mwaka uliofuata 2019, Kigoma ilipanda kidogo kufikia orodha ya 20. Hata hivyo, katika matokeo ya mwaka jana, NECTA haikufanikiwa kutoa mpangilio wa ufaulu kimkoa.

Je, katika mwelekeo uendako mkoa utajinasua kutoka daraja hilo la chini? Ni kitendawili ambacho majibu yake yanabakiza maswali kwa wanafunzi, wazazi, wadau wa elimu, viongozi na wakazi mkoani.

**DODOSO ZA SHIDA**

Said Magoma, ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwibuye wilayani Kasulu, anayetaja sababu za mwendelezo wa matokeo duni, inaanzia kwa jamii kutokuwa na mwamko chanya wa elimu, wakishindwa kutimiza wajibu wao wa kumsaidia mtoto kujisomea akiwa nyumbani.

Uzoefu unaonyesha, kumekuwapo utaratibu wa wazazi kuwaachia watoto majukumu ya kutunza familia wakiishi peke yao nyumbani, wenyewe wanapohamia mashambani.

"Watoto wanapewa majukumu makubwa yanayowazidi umri, yaani unakuta mzazi anamtumia mtoto kujiongezea kipato kwa kufanya shughuli za biashara katika masoko ya usiku," anasema mwalimu huyo.

Pia analalamika kwamba zimefanyika jitihada kubwa kuboresha elimu mkoani humo, lakini shule za vijijini zinahitaji msaada zaidi wa kupata mazingira bora ya kusomea, kwani ndiko zimekuwa zikifanya vibaya.

Utafiti wa Kujipima kwa Njia ya Kujifunza Afrika unaoratibiwa na Chuo Kikuu cha Aga Khan kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, umebaini kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika shule za msingi, kunakosababishwa na kutokuwapo uhusiano mzuri kati ya walimu na wanafunzi.

Octavia Lutasha, Mwalimu Mkuu katika Shule ya Msingi Majengo iliyopo katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, anasema wanafunzi wengi wanakosa utulivu darasani kwa sababu ya uhaba wa vifaa vya kufundishia na madarasa, hivyo kuathiri ufaulu katika mitihani.

"Mazingira ya mwalimu kufundisha darasa la watoto 200 ambao baadhi yao wamekaa chini, inachangia kushusha ufanisi wa ufundishaji na kufikia malengo kwani mwongozo wa Wizara ya Elimu unaelekeza darasa moja liwe na wanafunzi 45," anasema.

Mwalimu, Lutasha anashauri kuwa wazazi na serikali wanapaswa kufanya kazi kwa karibu, ili kutatua changamoto zinazowakumbuka wanafunzi shule za msingi.

**KIGOMA WAJIPANGA**

Ofisa Elimu Mkoa wa Kigoma, Paulina Ndigeza, anasema wameweka mkakati wa kukabiliana na matokeo hayo mabovu, hatua itakayosaidia kufuta historia hiyo na kuwezesha wanafunzi wengi kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya kuhitimu darasa la saba.

INAENDELEA UK.14

UCHAMBUZI

MARTHA MWASYEBA
NA ZUWENA SHAME

# Mtandao jamii, kirusi kinachotafuna kizazi kilichopo kwa kasi ya kutisha

- Watoto wanakua kuliko kasi ya umri
- Simulizi za madaktari nazo zinashtua

DUNIA ya karne ya 21 inatawaliwa na sayansi na teknolojia. Moja ya matunda ya maendeleo hayo ni kumshamiri mitandao ya kijamii. Ni manufaa ambayo pia yana sura hata kugeuka tatizo.

Sasa inabeba haiba ya kirusi hatari kitakachoangamiza kizazi. Watoto wadogo wamekuwa wataalamu wa teknolojia hiyo, kabla hata ya kuufikia umri sahihi. Si ajabu akakutwa wa miaka mitatu hajui kusoma, lakini ana uelewa fika wa 'you tube' inakopatikana na ilivyo.

Watoto wanajazana kifuatilia 'facebook, twitter, instagram' wakipekua na hakuna njia ya kuzuia, kuhusiana na umri wao.

Huko kwenye mitandao hiyo pamejaa habari nyingi zisizofaa kutoka kila upande wa dunia. Muhimu kwao ni kuona uwezekano kukawekwa 'kifurushi' washuhudie mambo hayo yanayojiri mabaya kwa mazuri.

Ni kawaida mtoto yuko tayari kukosa chakula, lakini akalilia mno kupatikana 'kifurushi' cha kumwezesha aone maudhui ya mtandaoni.



Wanafunzi wakitumia huduma za mtandao. **PICHA: MTANADAO**

### KUTOKA KWA WAZAZI

Nipashe ilifanya dodosa kupata picha ya uhalisia uliopo watoto 'kuzama' zaidi mitandaoni, wanakokutana na magumu yasiyowafaa.

Lusajo Fadhili, ni sehemu ya wazazi na walezi, mwenye ufafanuzi kwamba: "Mitandao ya kijamii si mibaya, lakini inaposhindwa kutumika vizuri, inateketeza mno kizazi chetu, kwani kuna vikundi vilivyokosa maadili, vinatumia mitandao ya kijamii kueneza mienendo yao.

"Hapa nagusia sana 'porn groups' na zile zinazojihusisha mapenzi ya jinsia moja. Zote hizi zimejizolea umaarufu na athari kubwa kupitia mitandao ya kijamii. Lakini, zaidi mitandao ya kijamiii imekuwa na mchango mkubwa kwa kulemaza watoto na kuwa chachu ya uvivu.

"Asilimia kubwa ya watu wanatumia muda mwingi humo na kusahau kufanya yanayowapasa kufanya, hata kujifunza kazi za mikono kama kupika, kufua na kupalilia, hata bustani. Matokeo yake tunazidi kuongeza kizazi cha wavivu na tegemezi.

"Nikisema tegemezi nina maana kwamba watoto wengi wa kizazi hiki hawajui kazi yoyote zaidi, zote wanafanyiwa na wafanyakazi wa ndani yaani vijakazi," anaeleza Lusajo.

Mwingine ni Peter Nicholous, anasema mitandao hiyo ambayo vina vyanzo vya ugenini, vimewateka mwanafunzi hata wapo shuleni, anafikiria atakavyofikia mitandao arudipo nyumbani.

Anaeleza dhana inayowateka, inajumuisha mada iliyojiri, mathalani usiku uliopita, ilhali ana mahitaji mengi ya masomo ambayo ni wajibu wake mkuu wa sasa kijana huyo.

Lingine analitaja ni pale mitandao ya kijamii inaposababisha kuingizwa utamaduni wa kigeni hasa kutoka nchi za Magharibi, hali inayochangia kuiteka jumuiya ya waangaliaji.

Ni hali anayoitaja kufika mbali, watoto wanatumia muda mrefu mitandaoni, wanadhurika katika afya ya mwili, ikiwamo macho na saikolojia zao, ushuhuda ukiwapo katika maeneo ya matibabu.

Winnie Nkya, mkazi wa Mbezi Makabe Dar es Salaam, anashangaa kwamba, haina mipaka kwa anayestahili na asiyestahili, jambo linalounda jamii kuelemewa na fikra duni au isiyofaa kulingana na umri ikiifikisha jamii pabaya.

Sunday Kasyupa, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ana mtazamo uliojaa mantiki ya kitaaluma, akisema: "Maarifa yanaweza kufanikisha kizazi kufika katika tumaini lake, kama kizazi kitapata taarifa zilizo sahihi.

"Ndani ya mitandao ya kijamii kumekuwapo wimbi kubwa la taarifa zisizo sahihi, ambazo kwa kiwango kikubwa zimeathiri kizazi chetu, kwa maana taarifa zisizo sahihi ni uharibifu wa Taifa."

Joseph Mrimi, anayeishi Buza kwa Mpalange, Dar es Salaam, anasema ongezeko kubwa la matumizi ya mitandao ya kijamii, yanaathari watoto wanaoupa kipaumbele kuliko masomo yao.

Akiwa na ufafanuzi kama walivyo baadhi ya watangulizi, anasema matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yanafikia athari za kiafya na kisaikolojia, mtu kuongezeka uzito kupita kiasi, kwa sababu wana muda mrefu wa kukaa.

Daktari Aliko, kutoka Hospitali ya Rufani Mbeya, anaeleza mitandao ya kijamii imechangia kuongezeka magonjwa ya akili, kwa sababu ya msongo wa mawazo.

Anasema, asilimia kubwa ya walioko katika mitandao ya jamii, wanaonyesha kuwa maisha bora na ya hali ya juu, hivyo waonaji wanapoakisi na maisha yao, wanajihisi hawana bahati ya mafanikio, sehemu kubwa wakiwa vijana.

Kwa mujibu wa Daktari Aliko, ndio unakuwa mwanzo wa kujikita katika vilevi kama bhangi na mihadarati, hali inayoteketeza kizazi kilichopo.

> "Mitandao ya kijamii au 'smart phone' ni kitu kigeni si kwa watoto tu, bali hata watu wazima. Mwanzo hatukuwa tunajua hivi vitu hivyo, elimu ya jinsi ya kudhibiti ni hafifu kwa watu walio wengi.

Anasema, hivi sasa kuna vijana wengi wa jinsia zote hujiingiza katika dhana ya kuendekeza mapenzi na wenye umri uliowazidi, baadhi wanalingana na wazazi wao, darasa kuu ni mtandao wa jamii, katika tamaa ya kutaka kupata wasivyomudu kuvipata kupitia juhudi binafsi.

### NINI KIFANYIKE?

Katika uhalisi unaotawala jamii ni katika changamoto, kuanzia jumuiya wataalamu mbalimbali, wakiwamo walimu na viongozi wa kiimani, wako katika mtihani wa kuwapatia elimu ya kutosha vijana.

Rai kuu ni kwamba, wanapaswa kuelewa mipaka ya ukweli wa maisha yao na mitandao, kwani kuna hatari wakashindwa kuzifikia ndoto zao, kwa starehe za muda mfupi.

Nchini, hasa katika baadhi ya miji mikubwa kama ilivyo jijini Dar es Salaam, huku mkazi wake, Mathias Philipo, anakiri mkazi au walezi wenzake, wanakosa elimu sahihi ya kudhibiti matumizi hayo kwa watoto wao.

"Mitandao ya kijamii au 'smart phone' ni kitu kigeni si kwa watoto tu, bali hata watu wazima. Mwanzo hatukuwa tunajua hivi vitu hivyo, elimu ya jinsi ya kudhibiti ni hafifu kwa watu walio wengi," anasema.

Philipo anasema, wazazi na walezi ndio wenye jukumu la kudhibiti nyenzo za mitandao jamii na tatizo linalojitokeza awali ni kukosekana maandalizi ya wahusika kudhibiti.

"Simu ni muhimu sana, ni msaada mkubwa kwa jamii kama itatumiwa ipasavyo au chanya na kuleta maendeleo na mabadiliko katika jamii husika," anadokeza Philipo na kuongeza:

"Lakini, mwingiliano kwa wazazi na walezi, je, wao wenyewe wanaitumia vipi? Maana watoto huiga kutoka kwa wazazi na walezi wao," anasema, huku akitaja eneo kubwa la madhara ni katika matumizi ya simu za kisasa, maarufu 'smart phone'

Mzai huyo anahitimisha hoja kwa hatua iliyofikiwa, mtoto anamilikishwa simu katika umri mdogo, akishirikishwa vikao vya familia kupitia matumizi ya simu, jambo linalozuia mipaka ya washiriki.

ELIMU

NA KHADIJA KALILI

# Mchungaji aandika kitabu chenye somo kamili linalofanikisha ndoa

• Darasa jipya analofananisha na kibubu • Asema upendo mzizi, uvumilivu wake ziada • Aorodhesha staili za kumnasa mwenza

WENGI wetu tunaingia kwenye ndoa tukiwa na tumejaza mawazo na kiu moyoni mwetu ya kwamba ndoa ni kitu kizuri sana tena kitamu sana.

"Tunawaza kwamba ndani ya kibubu hiki kiitwacho ndoa, kuna kila aina ya furaha na maliwazo kuna kila aina ya tulichowahi kukisikia kukitamani kama vile urafiki, mapenzi, kujaliana na ukaribu," anasema Mchungaji Daniel Lema.

Katika ufafanuzi wake kuhusu kitabu alichoandika kiitwacho 'Tunda la Ndoa' anaendelea kueleza: "Ukweli ni kwamba haya yanaweza kuwa ni mawazo matupu tu. Hiki kibubu kiitwacho ndoa, huanza kikiwa kitupu hakina chochote ndani yake, inayolazimu kuweka kitu kabla ya kutoa kitu.

Ni maudhui yatokayo na andiko la kitabu, pia kauli yake Mchungaji Lema, ni kwamba msukumo kufanya hivyo, akiwalenga walio katika ndoa na kinachowagusa katika ukweli wa maisha yao.

### DARASA NYUMBANI

Anataja mambo kama kutiana moyo, kujaliana, kusameheana, kuhurumiana au kusifiana hazikutwi ndani ya ndoa, bali wahusika hao huziingiza na kuzidumisha baada ya kuungana.

Mchungaji huyo wa Kanisa la Power of God, lililoko Buyuni Chanika, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, anatumia tamathali kwamba wawili hao wa jinsia tofauti wanapoungana, makusanyo ya mazuri yao yanaingizwa katika kibubu kimoja na hawapaswi kuchukua zaidi ya walichokikusanya, kwani kitabaki kitupu.

Katika andiko lake, anasisitiza uaminifu daima una matokeo



Mchungaji Daniel Lema. **PICHA: KHADIJA KALILI**

> Ndoa ni lazima iheshimiwe na watu wote...

sahihi, jambo ambalo limekuwa gumu kwa wanandoa, akidokeza sababu mojawapo ni baadhi kushindwa kuteua wenza sahihi.

Mchungaji Lema anajikita katika rekodi inayotolewa na wakala inayowajibika na vizazi, vifo, ndoa, talaka na kuasili watoto mapema mwaka huu, ni kwamba kuna ongezeko la talaka nchini.

Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa pia kitabu hiki ni maalumu kwa kila anayetamani kuwa na ndoa nzuri na anawataka wote kukisoma ili waweze kuelewa ujumbe ambao upo ndani ya kitabu hiko.

Mchungaji Lema anasema, ameandika kitabu hicho kutoa darasa kwa wale ambao hawajaingia kwenye maisha ya ndoa, wapate maarifa namna ya kumpata mume au mke sahihi maisha na namna ya kupambana na magumu yanayoweza kujitokeza njiani.

"Unapoingia kwenye ndoa ndipo utakutana na mambo ambayo utayafanya kama wajibu wako wewe mwanandoa," anasema.

"Najua kuwa ni agizo la Mungu. Kwenye ndoa, mume kumpenda mke wake na mke kumtii mume wake. Misingi hii miwili ndiyo imebeba agano kubwa la ndoa na mkiweza kukumbushana kila mara kile kiapo ambacho mlikifanya.

"Ni kawaida wanadamu kusahau mapema pale anapokuwa hajikumbushi mara kwa mara kile alichokisema au kukikiri kwa kinywa chake," anasema Mchungaji Lema.

Anarejea andiko la kiimani inayosisitiza mtu kutoishi pekee na ndoa ndiyo inawaunganisha rasmi na kitu pekee kinachowafunganisha watu wawili kuwa mmoja.

"Ndoa ni lazima iheshimiwe na watu wote na kuchukuliwa kama kitu cha thamani kwa kila mmoja, ndoa iliyo nzuri na baraka.

"Hakuna kitu kibaya katika maisha ya mwanadamu kama kuishi na mtu ambaye unamchukia kwenye ndoa. Jambo hili linaweza kusababisha msongo wa mawazo, hasira na chuki kwenye maisha ya mtu.

"Upendo kwenye ndoa ni kiungo muhimu muhimu sana, kinachoweza kupika na kufanya ndoa iwe yenye ladha nzuri. Upendo huo siyo upendo ule wa kawaida la hasha. Upendo wa kweli unapatikana kutoka kwenye chanzo cha upendo wa kweli," anasema.

Katika ufafanuzi wake, Mchungaji Lema anatumia mfano wa upendo wa mke unaangukia katika kumtii mume na kunyenyekea, hali inayochangia matokeo maisha yao kuwa ya furaha

"Ndoa nyingi zinaishia kuvunjika leo, kwa sababu wanandoa wengi wamekuwa wavivu wa kufuata yale ambayo yanatakiwa yatekelezwe... kwani ndoa siyo kwa ajili ya watu wavivu au walegevu, " anasema.

### UNAMNASAJE MWENZA?

Mchungaji Lema, anasema kuwa mara nyingi wakati mtu akiwa katika uhusiano wa uchumba si rahisi sana kugundua udhaifu wa mtu aliye mbali nawe muda wote.

" Nasema haya, kwa sababu kuna majibu mengi sana ya ndoa yako ambayo ukisoma kuelewa na kufanyia kazi, utakuwa mwenye ndoa yenye furaha na amani tele," anasema na kuhitimisha kwa kauli:

"Kuna neno moja linapendwa sana kutumiwa na watu wengi kuwa 'maisha ya ndoa ni uvumilivu na kuvumiliana.' Neno 'uvumilivu' likisimamiwa peke yake halina mantiki.

"Kwani uvumilivu palipo machafuko? Si kweli, bali maisha ya ndoa ni upendo, amani, uaminifu na juu ya haya yote lazima uwe na maarifa juu ya ndoa yako."

## Shule za Kigoma katika janga la 'kumi bora' kuanzia mkiani

INATOKA UK.12

Anataja mikakati hiyo, inajumuisha ufuatiliaji wa karibu wa mwenendo wa ufundishaji kwenye shule mbalimbali za mkoa, utakaokuwa unafanywa na watendaji wa serikali wanaohusika, pia kutoa motisha kwa walimu.

"Mimi naamini matokeo haya kuna uzembe unafanyika mahali hivyo sasa kila mtu kuanzia mzazi nyumbani ahakikishe anatekeleza wajibu wake," anasema Ofisa Elimu Ndigeza.

Anaeleza kuongeza kiwango cha ufaulu walimu watatakiwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo, kwa kuhakikisha hakuna kipindi kinachopita, bila ya wanafunzi kufundishwa pamoja na ufuatiliaji kutekeleza mitaala shuleni.

Ofisa Elimu anasema, wameunda kamati za taaluma zinazofuatilia mwenendo wa elimu kwa kila wilaya, jukumu lake kubwa ni kufuatilia ufundishaji, utoaji mazoezi na mitihani ya kuwapima wanafunzi kila mwezi.

Ufuatiliaji huo utaendana na utoaji ripoti na kuchukua hatua za kimaadili kwa watakaobainika kutokutimiza wajibu wao ikiwamo kutokupandishwa madaraja na kushushwa madaraja.





## 'Watoto wenye ulemavu wakandamizwa na mila potofu'

**Na Peter Mkwavila DODOMA**

WADAU wa Elimu Jumuishi mkoani Dodoma, wamesema mila na desturi potofu zinaendelea kufanywa kwa watoto wenye ulemavu na wanajamii, hali inayoendelea kuwa kero kwa kuwakosesha haki zao za msingi kama ilivyo kwa watoto wengine. Baadhi ya haki hizo ni kukosa elimu, matibabu, miundombinu rafiki, burudani, nafasi za uongozi, kutoa maoni yao na kunyimwa fursa mbalimbali za kuchangia kwenye jamii ikiwamo familia.

Wadau hao walisema hayo wakati walipokuwa wakizungumza kwenye mafunzo ya mradi wa Elimu Jumuishi ulio chini ya Kanisa la FPCT kwa ajili ya viongozi wa asasi za kiraia kuhusu ushawishi na utetezi kwa watoto wenye ulemavu iliyofanyika jijini hapa.

Richard Mwaga, kutoka Shirika lisilo la kiserikali la AFNEt, alisema bado kuna mila na imani potofu miongoni mwa wanajamii zinazowanyima haki watoto wenye ulemavu na kuwasababishia kuendelea kuteseka na kuwa tegemezi katika maisha yao.

Alisema kuna umuhimu na ulazima kwa upande wa serikali na asasi mbalimbali, watu binafsi kutoa elimu kwa wanajamii na familia wanazoishi watoto hao ili kuwakomboa na waweze kupata haki zao za msingi ikiwamo elimu pamoja na mahitaji yao muhimu.

Kwa upande wake, Erick Mapunda, kutoka Tanzania Cheshira Foundation, alisema watoto wenye ulemavu wana uwezo mkubwa wa kuongeza uchumi kwa taifa, ikiwa watapatiwa fursa mbalimbali za kuwezeshwa kielimu.

Alisema kwa kushirikiana na familia, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuna uwezekano mkubwa wa kuwafanya watoto hao kujisimamia wenyewe kwenye sekta mbalimbali, familia zao na maeneo ya serikalini.

Naye Mwanasheria wa kujitegemea, Fredrick Mkatambo, alisema watu wenye ulemavu wanapaswa kupewa fursa sawa katika masuala yote ya kimaisha kama ilivyo kwa wengine.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo ya ushawishi na utetezi wa elimu jumuishi, alisema kuna umuhimu wakutenga masuala ya watu wenye ulemavu pamoja na kuwajumuisha na jamii ya kawaida ili waweze kupata haki za kimsingi.

Alisema kwa upande wa watoto wenye ulemavu ni vizuri nao wakapata haki sawa na wengine hasa katika upatikanaji wa elimu wa mahitaji mengine tofauti na ilivyo sasa wengi hawapatiwi fursa zao zinazostahili kama wanadamu.

Alisema nchi nyingi duniani zimekuwa zikizungumzia misingi ya haki za binadamu ya wote kuwa na haki ya kuwa huru na kwamba ni muhimu kujali maslahi yao ya watoto wenye ulemavu ili waweze kufurahia kupata elimu kama watoto wengine.

"Hata kwenye shule zetu tunatakiwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto kujenga miundombinu sahihi, vyoo rafiki hayo ndiyo maslahi mapana kwa mtoto kwa mfano pale wilayani Bahi tunatengeneza chumba kimoja kwa ajili ya wasichana kujisitiri ili wanapofika kwenye kipindi cha hedhi wapate sehemu ya kujihifadhi ndiyo maslahi ninayosemea hapa," alisema.

# Watumishi NEC watakiwa kuzingatia sheria, kanuni

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Mbarouk Salum Mbarouk, amewataka watumishi wa tume hiyo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za serikali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Jaji Mbarouk, alitoa ushauri huo jijini hapa wakati wa kufungua mkutano wa kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo.

Alisema ni vyema wafanyakazi hao wakazingatia kutokana na umuhimu wao katika kutekeleza dira na malengo ya tume.

"Pamoja na changamoto mnazokutana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yenu manatakiwa kutambua ninyi ndio mnabeba dira na malengo ya tume," alisema.

Alisisitiza umuhimu wa watumishi hao kushirikiana kutekeleza majukumu yao ili kufanya kazi kwa ufasaha na kusaidia kupata mafanikio kwenye malengo ya tume.

"Ninyi mna nafasi kubwa katika kuwafahamisha na kuwaelimisha wafanyakazi wenzenu ili waweze kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali.

"Tume inaamini kwamba ili mtumishi aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha ni muhimu kupata ushirikiano kati yake na kiongozi wake na watumishi wenzie," alisema.

Pia aliwasihi watumishi wa Tume kuwahudumia wateja wao wa ndani na nje kwa weledi na kwa wakati na kwa kufanya hivyo kutajenga taswira nzuri kwa Tume.

Aliwapongeza watumishi hao kwa kutekeleza majukumu yao ya kikatiba katika kusimamia na kuendesha uchaguzi mkuu na uandikishaji wapigakura kwenye daftari la kudumu.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Mahera, alisema mkutano huo wa baraza ni wa kwanza na moja ya ajenda ni kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa bajeti ya mwaka 2021/2022 wa Tume.





Wanunuzi wa mahindi wakiyapakia kwenye gari katika soko la kimataifa la mahindi Kibaigwa Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma juzi, wauzaji wa mahindi kwenye soko hilo wamekuwa na malalamiko ya kukosa soko la mazao yao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu aonya upokeaji taarifa za uzushi

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

ASKOFU Mkuu wa Pentekosti Christian Church International Tanzania, Thomas Kiula, amewataka Watanzania kujiepusha na upokeaji wa taarifa zisizo sahihi zinazotolewa na baadhi ya mitandao ya kijamii.

Alitoa tahadhari hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa na kuwataka Watanzania kuwa makini na taarifa za upotoshwaji.

"Serikali yetu ina utaratibu wake wa utoaji taarifa kwa kuwa ndio wasemaji na sio vinginevyo hivyo ninawasihi Watanzania wezangu kuwa makini na hii mitandao ambayo imekuwa ikitoa taarifa zisizo na ukweli na nyingi ni za udanganifu na upotoshaji," alisema.

Hata hivyo, aliiomba serikali kutowafumbia macho kwa wale watakaobainika kutoa taarifa hizo ikiwa ni pamoja na kufungia vyombo vyao vinavyotumika kwenye upotoshaji huo.

Pia aliwataka viongozi wa madhehebu ya dini kuendelea kutoa elimu kwa waumini wao ili waweze kuondokana na upotoshwaji huo kwa kupitia simu zao za mikononi.

Alisema, elimu hiyo itawawezesha kujiepusha na mkono wa serikali ambao umekuwa ukifanya kazi zake kuwabaini wanaosambaza taarifa zisizo na ukweli kwa kupitia mitandao ya kijamii.

Askofu Kiula alisema viongozi wa madhehebu ya dini wananafasi kubwa ya kuwaelimisha waumini hao kujilinda na matukio yanayoweza kuichafua serikali na wao wenyewe bila kujitambua.

"Sisi viongozi wa madhehebu ya dini tuna kila sababu ya kuwaelimisha waumini wetu kuhusiana na masuala mbalimbali yanayojenga taifa letu badala ya kuiachia serikali peke yake kutoa elimu hiyo muhimu kwa waumini wetu," alisema.



HABARI MBEYA

# Wachimbaji watumia mabomba kuwasiliana

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu wilayani Chunya wanalazimika kuwasiliana kwa kutumia mabomba kati ya wanaokuwa juu na wanaozama kwenye mashimo kutokana na kukosa teknolojia za kisasa za kuwasiliana.

Wakizungumza wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kudo Mathew, wachimbaji hao waliiomba serikali iwasaidie teknolojia itakayowafanya wawasiliane kirahisi.

Mmoja wa wachimbaji hao, Benard Mwalukasa, alisema miaka ya nyuma walikuwa wanachimba madini yanayopatikana kina kifupi kutokana na teknolojia duni walizokuwa wanazitumia tofauti na sasa zimekuwa za kisasa.

Alisema kwa sasa wanachimba kwenye mashimo yenye urefu wa kuanzia mita 70 mpaka 100 urefu ambao unahitaji njia za kisasa za mawasiliano akidai kuwa katika eneo hilo mawasiliano ya simu za mkononi ni ya shida.

"Tunaomba serikali itusaidie angalau tuwe tunatumia 'radio call' maana kwa sasa tunalazimika kuchomeka mabomba kutoka juu ya shimo mpaka chini ili litusaidie kuwasiliana kati ya wanaozama kwenye mashimo na wanaokuwa juu ya teknolojia ambayo ni duni sana," alisema Mwalukasa.

Naye Yotham Mwangupila, alisema mawasiliano ni muhimu kwenye sekta hiyo kwa sababu wakati mwingine yanatokea matatizo ya migodi kuporomoka na kufukia watu.

Alisema wakitumia mbinu za kisasa za mawasiliano ni rahisi kuwasiliana linapotokea tatizo na kwa mawasiliano ya kawaida.

Akijibu maombi ya wachimbaji hao, Naibu Waziri, Mathew alisema serikali haiwezi kuwanunulia simu wananchi na badala yake huwa inatengeneza miundombinu.

Aliwataka wachimbaji hao kujinunulia vifaa vya mawasiliano kwa maelezo kuwa wanajiingizia fedha nyingi kutokana na shughuli hiyo na hivyo ni lazima wajitengenezee mazingira rafiki ya utendaji kazi.

"Sitaki kuwa mnafiki, kuna lile ambalo ni jukumu la serikali na yapo ambayo ni majukumu ya mwananchi mmoja mmoja, mnachimba dhahabu, mnauza na mnapata fedha, sasa mnashindwa nini kuingia madukani na kununua hizo radio call?" Alihoji.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ili kuwarahisishia wananchi mawasiliano na kuwataka wachimbaji hao kuchangamkia fursa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon, aliwataka watoa huduma za mitandao ya simu kuwatembelea wananchi kwenye maeneo yao mara kwa mara ili kutatua matatizo ya kimawasiliano yanayowakabili. Alisema kitendo cha wananchi kuwa na uhitaji wa mawasiliano ni fursa kwa kampuni hizo kupanua huduma zao kwenye maeneo yenye uhitaji ikiwamo ya Wilaya ya Chunya ambayo shughuli kubwa za kiuchumi ni kilimo na uchimbaji.

Alisema huduma ya fedha za mtandao ni shida katika maeneo hayo na kuziomba kampuni za simu kuweka mawakala kwenye maeneo hayo ili wawahudumie wananchi.




Moja kati ya pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) ikiwa imebanwa na magari mawili likiwamo lenye namba za usajili za serikali baada ya dereva wa bajaji hiyo, kuendesha bila kuzingatia usalama. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Asilimia 90 ya ngano inaagizwa toka nje

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ASILIMIA 90 ya zao la ngano inayotumika nchini inaagizwa kutoka nje ya nchi kutokana na mwamko mdogo wa wakulima kuzalisha zao hilo pamoja na teknolojia duni za uzalishaji.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya uzalishaji wa mbegu za zao hilo katika mashamba ya taasisi hiyo.

Alisema mahitaji ya ngano nchini ni tani 1,000,000, lakini uwezo wa uzalishaji ni tani 100,000 pekee, huku akidai kuwa hali ya hewa ya maeneo mengi nchini inafaa kwa kilimo cha zao hilo na kinachotakiwa ni hamasa.

Alisema kwa sasa wanaendelea na uzalishaji wa mbegu za zao hilo ili kutekeleza agizo la Rais Dk. John Magufuli la kuhakikisha Tanzania inajitosheleza kwa zao hilo ifikapo mwaka 2025.

"Sasa hivi mtu akishika maandazi au chapati 10 ni moja pekee ndio inakuwa imetengenezwa kwa ngano zinazozalishwa hapa nchini na mengine yanayobaki ni kutoka nje, sasa tunataka tubadili hali hii ili angalau kiasi kikubwa tuzalishe sisi," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema pia inafanya kazi ya kuelimisha wananchi kuhusu kilimo bora cha zao hilo ili kuongeza tija zaidi na kufikia lengo la kujitosheleza.

Mtafiti wa ngano wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Rose Mongi, alisema kuanzia msimu huu taasisi hiyo inakusudia kuzalisha mbegu za ngano kwa wingi, kuzisambaza kwa wakulima ambao watazalisha ili kufikia lengo la serikali.

Dk. Mongi ambaye ni mratibu wa zao hilo, alisema Tanzania ilianza kuzalisha zao hilo zaidi ya miaka 100 iliyopita, lakini uzalishaji uko chini kutokana na hamasa kuwa ndogo kwa wakulima na kusisitiza kuanzia sasa wananchi watapata hamasa kubwa.

Alisema mpaka sasa zipo mbegu bora ambazo taasisi hiyo imezalisha na kuidhinishwa kuanza kusambazwa na zingine wanaendelea na utafiti ili nazo zisambazwe kwa wakulima kulingana na hali ya hewa ya maeneo wanayoolima.

"Ili kuwahamasisha zaidi wakulima, tayari tumeanzisha mashamba darasa kwa ajili ya kuwafundishia wakulima wadogo wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na tunahamasisha zaidi wawe kwenye vikundi ili iwe rahisi kuhudumiwa," alisema Dk. Mongi.

Alisema endapo wakulima watakuwa pamoja kuna uwezekano wakasaidiwa na huduma za kupanda na kuvuna kwa kutumia mashine za kisasa ambazo tayari serikali imezinunua.

Baadhi ya wakulima waliokwenda kupata mafunzo ya kilimo cha zao hilo katika kituo hicho, waliomba elimu hiyo iendelee kutolewa ili uzalishaji uongezeke na kufikia kujitegemea kwa zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Enike Kagula, alisema wakati serikali inapohamasisha wananchi kulima zao hilo ni vyema pia ikawahakikishia upatikanaji wa soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Alisema baadhi ya wakulima wa mazao mengine ya nafaka wanalalamika kukosa soko mara kwa mara na kwamba kuna uwezekano uzalishaji wa ngano ukiongezeka pia soko likashuka.

# Walalamikia mawakala wa simu gharama za ziada

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

WANANCHI wilayani Chunya wamelalamikia tabia ya mawakala wa mitandao ya simu kuwatoza fedha za ziada wanapokwenda kuweka fedha kwenye simu zao kinyume na sheria za nchi bila kuchukuliwa hatua.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi na wananchi wa kijiji cha Itumbi wilayani Chunya mbele ya Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew, wakati alipotembelea kijijini hapo kukagua hali ya upatikanaji wa mawasiliano ya simu katika eneo hilo.

Jumanne Mwesigwa alisema katika kila Sh. 100,000 ambayo mwananchi anakwenda kuweka kwenye simu, anatakiwa kuongeza Sh. 3,000 kama gharama ya kupewa huduma hiyo.

"Ukienda na laki moja unatozwa shilingi elfu tatu ya ziada na kadri fedha inavyoongezeka pia unatakiwa kuongeza fedha, kwa mfano ukitaka kuweka Sh. 300,000 unatozwa Sh. 10,000 hivyo tunakuomba waziri utuambie kama ni halali kufanyiwa hivyo na hawa mawakala wetu?" Alisema Mwesigwa.

Alisema pia wakipoteza laini zao za simu au wakihitaji kusajili laini mpya wanatozwa fedha nyingi kuliko ilivyo kwa wakazi wa mijini.

"Ukipoteza laini na ukataka kuirudisha kupitia mawakala wetu unatozwa Sh. 10,000 na ukitaka kusajili laini mpya kwa alama za vidole wanakutoza Sh. 5,000, hili nalo sisi tunaona kama wanatuonea kwa sababu ukienda kupata huduma hiyo mjini unatozwa Sh. 1,000 tu," alisema Mwesigwa.

Akizungumzia suala hilo, Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Asajile John, alisema huduma ya kusajili laini ni bure na mpya inauzwa Sh. 1,000.

"Laini ya simu ndiyo inayouzwa kwa gharama ya Sh. 1,000, mwananchi ukishainunua unatakiwa kusajiliwa bure, hata kurejesha laini iliyopotea gharama yake ni hiyo hiyo," alisema Asajile.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, aliagiza mitandao yote ya simu kuwashughulikia mawakala wao wanaokwenda kinyume na sheria za nchi kabla hajachukua hatua dhidi ya kampuni hizo za simu.





# Elimu kwa wawekezaji wazawa yaombwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeombwa kutoa elimu ya sheria na kanuni kwa wawekezaji wazalendo ili kuepuka hasara wanayoweza kuipata wakati wa kuendesha miradi yao kutokana na kutokufahamu vema sheria na kanuni hizo za uwekezaji.

Ushauri huo ulitolewa jana na baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Bwejuu Wilaya ya Kusini Unguja, kufuatia uharibifu mkubwa uliyofanywa katika hoteli ya Palm Beach Inn iliyopo kijijini hapo.

Wananchi hao walisema asilimia kubwa ya wazawa hawana uelewa juu ya mikataba ya uwekezaji hasa pale wanapokodisha miradi yao na hivyo kujikuta wakipata hasara ya kuharibiwa kwa mali zao.

**Wananchi hao walisema asilimia kubwa ya wazawa hawana uelewa juu ya mikataba ya uwekezaji hasa pale wanapokodisha miradi yao na hivyo kujikuta wakipata hasara ya kuharibiwa kwa mali zao.**

Wakitolea mfano hoteli hiyo ya Palm Beach Inn, wananchi hao walieleza kuwa baada ya wamiliki wa hoteli hiyo kuikodisha kwa wawekezaji, makubaliano yao hayakuzingatiwa na hivyo kujikuta wakipata hasara.

Walisema kabla ya hoteli hiyo kukodishwa kwa mwekezaji mwingine, ilikuwa inafanya kazi vizuri, lakini kwa sasa imesitisha shughuli zake na kusababisha wananchi waliokuwa wakifanya kazi humo kukosa ajira.

Ali Ameir Chamnda, alisema serikali inapaswa kufuatilia mikataba ya wawekezaji wazawa wanayoingia na wawekezaji kutoka nje ya nchi ili kuwasaidia wasipoteze mali zao.

"Ni vema serikali kabla ya kuwapa vibali wawekezaji wawe wanawachunguza kwa sababu wapo baadhi yao ambao lengo lao siyo kuwekeza na badala yake ni kutaka kuhodhi maeneo kwa maslahi binafsi kupitia kichaka cha uwekezaji," alisema Chamnda.Naye Asma Abdalla alisema kuharibika kwa hoteli hiyo kumesababisha hasara kubwa kwa wananchi waliokuwa na ajira hapo.

"Tumepoteza ajira, mimi binafsi nilikuwa nasambaza samaki katika hoteli hiyo, lakini baada ya kuja mwekezaji mpya alisitisha, lakini ameifanya hoteli hiyo kuwa katika hali mbaya," alisema Asma.

Mmiliki wa hoteli hiyo, Mahfoudh Ali Mahfoudh, alisema waliingia mkataba wa uwekezaji na Javed Abid Jafferji wakishirikiana na Adnan Abrass kwa zaidi ya miaka mitatu lakini hakuna kilichofanyika mpaka sasa.

Alisema Mahakama ilishaamuru hoteli hiyo kurejeshwa kwa mwekezaji wake wa awali baada ya yule aliyekuwa amepewa kuiendesha kushindwa kutekeleza makubaliano ya kuiendeleza.

## Abdullah ataka miradi ya kilimo kupitiwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema ipo haja ya kuangaliwa upya miradi ya kilimo katika utekelezaji wake ili ilete tija kwa wananchi hususani wakulima.

Alisema mfumo wa sasa wa kuwatoza fedha wakulima kwa kuzingatia ushauri wa wafadhili katika baadhi ya miradi kuandaa mashamba yao utawabebesha mzigo kulingana na hali ya kipato cha kimaisha.

Hemed alisema hayo wakati wa ziara yake ya kiserikali katika wilaya mbalimbali za Zanzibar kuangalia miradi ya kijamii, serikali pamoja na kufuatilia changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Alisema serikali itaangalia kwa kina miradi yote sambamba na gharama zilizotumika ili ijiridhishe ili kuhakikisha inayofanyika ni ile inayoleta tija kwa wananchi.

Alisema serikali iko tayari kukaa pamoja na wananchi ili kujadili kero zinazowasumbua ikiwamo migogoro ya ardhi, sehemu za makazi, barabara na kwenye maeneo ya kilimo, ili kupata mwelekeo wa pamoja wa namna ya kutatua changamoto hiyo.

Aliwataka wananchi kuwa na subira wakati changamoto zao zinatafutiwa ufumbuzi na serikali.

Akizungumzia nishati ya umeme, Hemed aliutaka uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kujipanga vyema kibiashara na kwamba endapo atatokea mwekezaji kuonyesha mwelekeo mzuri serikali haitasita kumpa fursa bila ya kujali kwamba ZECO ni shirika la serikali.

Alisema lazima lijikite kupunguza malalamiko ya wananchi yanayojitokeza kila mara hasa umeme mdogo unasababisha kuwaletea hasara ya kuungua kwa vifaa vyao pamoja na urasimu wa upatikanaji wa huduma hizo kwa wale wateja wanaohitaji kuungiwa nishati hiyo.

Akizungumza na wananchi wa vijiji vya Tunguu, Machui, Kibonde Maji, Bambi Kijiwe Mtu na Bonde la Cheju waliosimama kumkaribisha wakati wa ziara yake ya Wilaya hiyo ya Kati, alisema serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi na tayari imeshajizatiti kuzipatia ufumbuzi.

Pia aliziimiza Halmashauri za Wilaya kuendelea kusimamia vyema na udhibiti wa mapato ya serikali.

Alisema haipendezi kuona uongozi wa halmashauri unajipangia vyema kukusanya mapato ya mwaka kwa asilimia 100, lakini matokeo yake ripoti zinazowasilishwa zinaelezea chini ya asilimia hiyo jambo ambalo huzorotesha ukusanyaji wa mapato ya serikali katika vianzio vyake vya taasisi za umma.

Akitoa taarifa ya serikali nya Wilaya ya Kati, Mkuu wa Wilaya hiyo, Marina Thomas, alisema kata 38 zilizomo ndani ya Wilaya ya Kati tayari zimefanikiwa kupata huduma za majisafi na salama kufuatia kuongezeka kwa miradi ya visima vitano vya maji safi na salama.

Marina alisema mafanikio hayo yamekwenda sambamba na upatikanaji wa huduma za umeme kwa kiwango kikubwa kutokana na miradi 12 iliyotekelezwa na wananchi wengi kunufaisha na nishati hiyo muhimu.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, akiangalia baadhi ya bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda cha nguo cha Basra, Mwembe Makumbi, alipofanya ziara ya ghafla kutaka kujua sababu ya kiwanda hicho kisitisha uzalishaji. Kushoto ni Meneja wa kiwanda hicho, Saleh Saleiman Hamad. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watendaji wakuu wasimamishwa kazi

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

WAZIRI wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, ameagiza kusimamishwa kazi watendaji wakuu wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Ole-Kengeja yenye urefu wa Kilomita 35, kutoka na fedha zilizotumika kutokuendana na ujenzi wa barabara hiyo.

Walioagizwa kusimamishwa kazi katika mradi wa barabara hiyo, ni msimamizi mkuu kwa upande wa Pemba, Injinia Amini Khalid na mratibu wa barabara hiyo Injinia Amina Mohamed Habibu.

Waziri alitoa agizo hilo katika majumuisho ya ziara yake katika barabara ya Ole-Kengeja na kuona baadhi ya kasoro zilizojitokeza wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

Baada ya kukagua alionyesha shaka katika ujenzi unaoendelea katika barabara hiyo na kwamba haukuwa wa kiwango kulingana na fedha iliyotumika.

Miongoni mwa kasoro ambazo alizibainisha katika barabara hiyo ni pamoja ujenzi usio ridhishwa wa makalavati, barabara kupasuka pasuka, kukosekana alama za barabarani, kukosekana kwa mitaro ya kupitishia maji katika barabara pamoja na mkataba wa ujenzi kuwa na mashaka.

Aidha, waziri alisema fedha zilizotumika ni za wananchi na hazilingani na thamani ya ujenzi, hivyo amewaagiza kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi.

Waziri huyo alisema watahakikisha miradi yote iliyomo kwenye wizara yao, wanaikagua kwa lengo la kujiridhisha juu ya matumizi ya fedha zilizotumika zinalingana na ujenzi husika na kwamba ikibainika kuwa na kasoro hatua zitachukuliwa. "Hii barabara imejengwa haraka haraka na haina kiwango nimeitembelea lakini ujenzi haulingani na fedha iliyotumika, lazima fedha za wananchi tuzionee huruma licha ya kuwa mimi sio mtaalamu," alisema Khalid.

"Pia kuna ukiukwaji wa mkataba wa ujenzi na nautilia shaka haukwenda hata kwa mwanasheri, ninataka mamlaka ya nidhamu kuwasimamisha kazi kwa mujibu wa sheria kupisha uchunguzi na baada ya kujiridhisha watawaachiwa, pamoja na hatua nyingine kufuata."

Alisema atahakikisha anaunda tume ya uchunguzi kwa ajili ya kujua tatizo hilo na kwamba ikibainika kuwapo kwa watu wengine ambao wameingia katika matatizo hatua kali zitachukuliwa.

Katibu Mkuu Wizara yaUjenzi Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Amour Hamil Bakar, alisema kwa sasa wanafanya tathmini ya madai ya fidia zote ambayo yapo wizarani na mengine ambayo yamekuwapo zaidi ya miaka 20, na kwamba wameamua kujipa muda ili kuhakikisha wanayamaliza.

Akizungumzia matengenezo, alisema watahakikisha maeneo yote ambayo barabara zimekatika wanayafanyia marekebisho, ili barabara ziwe katika hali nzuri.

"Maeneo mengi yapo ambayo yanahitaji kufanyiwa matengenezo ya haraka kabla ya mvua hazijaja, tutajitahidi kufanya ukarabati na kuwa katika kiwango kizuri," alisema Bakar.

Akizungumzia suala la agizo la kuwasimamisha kazi, aliseme watalitekeleza na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kama agizo la waziri lilivyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NTWA L MWANDEMANI** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S137/933** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MKWAWA mwaka 1996,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **SBR/RB/237/2000**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NTWA MWANDEMANI** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0534/0212** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ST. ANTHONY'S SECONDARY SCHOOL MBAGALA** mwaka 1993, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **SBR/RB/237/2000**

## TANGAZO LA MNADA

**TAN-GLOBAL VENTURES COMPANY LIMITED** kwa idhini iliyopewa na **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC)** itauza kwa mnada wa hadhara nyumba ilizo orodheshwa kwenye jedwali kwa eneo na tarehe tajwa hapo chini:

| JINA LA MDAIWA | NAMBA YA KIWANJA/KITALU | ENEO LILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| JOEL MARWA MATIKU | PLOT No.346 | BOMANI AREA-TARIME | 19/04/2021 |

**MASHARTI YA MNADA:** Mnunuzi aliyeshinda anatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano(25%) mara tu baada ya mnada kufungwa,na atakamilisha asilimia sabini na tano(75%) baada ya siku kumi na nne(14),Fedha hiyo isipolipwa ndani ya muda huo mnada utarudiwa bila kurudishiwa fedha ya awali.

**ABRAHAM SHEMPEMBA**
**Mkurugenzi Mtendaji**

Imetolewa leo tarehe 16/03/2021 na **TAN-GLOBAL VENTURES CO.Ltd, S.L.P 612, TANGA, abrahamshempemba@gmail.com 0715-752205, 0714-560080, 0692-693410**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEPHEN GATI MWITA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN CARAVAN** yenye namba za usajili **T956 AVU** engine namba **CC2663,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/141439/2021**

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**

**AT SAMORA AVENUE**

**PROBATED AND ADMINISTRATION CAUSE NO...17.... OF 2021**


**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MOSES JABIR KABOJOKA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR THE LETTERS OF ADMINSTRTION BY CHRISTINA BUGHALI KABOJOKA**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration)is made to the above named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 31 day of March 2021
Date at 03 this day of MARCH 2021




## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LONAGRO TANZANIA LIMITED** wanatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya FORD RANGER yenye namba za usajili **T 656 CKR** engine namba **SA2HPCY68179,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/146669/2021**

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Bobi Wine, wabunge 15 wakamatwa na polisi

**Kampala,** UGANDA

MWANASIASA wa Uganda ambaye alikuwa mgombea urais wa chama cha upinzani, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, amekamatwa katika mji mkuu wa Kampala.

Wakati Bobi Wine akikamatwa, alikuwa anaongoza timu ya wabunge kutoka Chama chake cha National Unity Platform, kufanya maandamano dhidi ya kukamatwa na kutoweka kwa wafuasi wake kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu, uliofanyika Januari.

Vikosi vya usalama vilifyatua vitoza machozi na kutawanya waandamanaji waliokuwa wameandamana na mwanasiasa huyo.



Bobi Wine na wanachama wengine wa chama hicho wakiwa wamekamatwa jana na polisi mjini Kampala, baada ya kufanya maandamano kupinga watu waliopotea kabla na baada ya uchaguzi. **PICHA: DAILY MONITOR**


Inasemekana kwamba waliokamatwa ni pamoja na wabunge 15.

Katika mkutano uliofanyika kupitia njia ya video, Bobi Wine alitoa wito kwa wafuasi wake kutumia njia za amani kuandamana dhidi ya matokeo ya uchaguzi, ambayo anaendelea kudai kuwa vikosi vya usalama vitoe wale wasiojulikana walipo.

Kukamatwa kwake kutokana na mkutano wa kampeni uliofanyika Novemba, kulianza siku mbili baada ya maandamano na watu zaidi ya 50 waliuawa.

Gazeti la Uganda la Daily Monitor, limeweka kwenye mtandao picha za Bobi Wine akikamatwa jana.

**BBC**



Anga la mji mkuu wa China, Beijing, jana lilifunikwa na vumbi la mchanga kufuatia dhoruba na upepo mkali, tukio ambalo halijashuhudiwa kwa muongo mmoja na kusababisha mamia ya safari za ndege nchini humo kufutwa. **PICHA: BBC**

## Mgambo waua wanajeshi 30

**Monguno,** NIGERIA

WANAMGAMBO wenye msimamo mkali wamewaua wanajeshi 30 wa serikali katika mfululizo wa mapigano, Kaskazini Mashariki mwa Nigeria.

Shirika la Habari la Reuters, lilisema kwamba usalama kote Nigeria, umezorota katika miezi ya hivi karibuni ikijumuisha ukanda huo.

Mashambulizi manne yalisababisha vifo vya wanajeshi 27 na wanamgambo wa kikosi cha raia 10, ikijumuisha mkuu wa kikosi, kwa mujibu wa Reuters.

Jeshi na msemaji wa wizara ya ulinzi hawakuwa tayari kujibu simu na ujumbe uliotumwa ili kutoa ufafanuzi wa habari za mashambulizi hayo.

Kundi la Islamic State West Province (ISWAP), ambalo lina ushirikiano na kundi la Islamic State (IS), limedai kuhusika na mashambulizi ya Ijumaa ya Monguno, kupitia shirika la habari la Amaq siku ya Jumamosi.

ISWAP limedai kuua wanajeshi 33 na kumkamata mmoja.

**VOA**

## 400,000 wauawa Syria kwa miaka 10

**London,** UINGEREZA

IDADI ya watu waliokufa kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Syria, imekaribia laki nne, tangu vilipoanza muongo mmoja uliopita.

Hadi sasa hakuna ishara ya vita hivyo kumalizika.

Kwa mujibu wa Shirika la Kufuatilia Haki za Binadamu la Syria, lenye makao yake nchini Uingereza, idadi kamili ya watu waliopoteza maisha yao kwenye vita hivyo ni 388,652 kufikia Machi, 13 mwaka huu.

Wengi katika waliopoteza maisha ni raia wa kawaida, miongoni mwao wakiwa ni watoto wadogo.

Mashambulizi yaliyofanywa na vikosi vya serikali ya Syria na makundi ya wanamgambo yanayoiunga mkono ndiyo yaliyoangamiza maisha ya watu wengi zaidi.

**DW**

# Museveni ajifikiria kuchanjwa AstraZeneca

**Kampala,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema bado anaangalia ni chanjo ipi atakayochomwa.

Katika hotuba yake jana, Rais Museveni alisema hajapata chanjo bado kwa kuwa yuko makini na ana ulinzi wa kutosha.

Pia mke wake, Janet Museveni, bado hajapata chanjo hiyo.

Wakati ikiwa ni siku chache baada serikali yake kuanza kutoa chanjo ya Oxford-AstraZeneca kwa wananchi.

Tayari marais wengine barani Afrika, wameonyesha kwa umma wakipata chanjo ili kuhakikishia usalama na ubora wa chanjo.

Mwezi uliopita Waziri wa Afya wa nchi humo, Jane Aceng, alikanusha taarifa kuwa rais na watu wake wa karibu walikuwa wanapokea chanjo nyingine kwa siri kabla ya taifa hilo kupokea chanjo rasmi.

Alitoa ufafanuzi baada ya gazeti la nchini humo la Daily Monitor na gazeti la Marekani la jarida la Wall Street.

Aidha, Rais Museveni alilitaka gazeti hilo kuomba radhi kwa kuandika barua kwenye kurasa ya mbele ya gazeti au atawafuata.

Uganda ina mpango wa kutoa chanjo kwa asilimia 49.6 ya idadi ya watu katika awamu ya kwanza.

Nchi hiyo ilipokea dozi 864,000 za chanjo kutoka Covax mapema mwezi huu na inatarajia kupokea nyingine 2,688,000 mwishoni mwa mwezi Juni.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# CAVANI, MARTIAL KUIWAHI AC MILAN




**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer ana matumaini ya kurudi kwa wachezaji wanne au watano kutoka chumba cha majeruhi, wakati Manchester United itakapocheza na AC Milan kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Europa hatua ya 16-bora keshokutwa, Alhamisi.

Kocha huyo wa United, Solskjaer anawatarajia washambuliaji wake, Edinson Cavani na Anthony Martial kuwa fiti.

Donny van de Beek, ambaye amekuwa nje ya dimba tangu Februari 22, pia anaweza kuwa tayari kurudi, huku Paul Pogba ambaye alicheza kwenye sare ya 3-3 dhidi ya Everton Februari 6, mwaka huu naye anaweza kuwapo kwenye kikosi.

Huku Marcus Rashford akiwa amesharudi dimbani baada ya kuumia kifundo cha mguu na alikuwamo kwenye mchezo wa ushindi wa 1-0 dhidi ya West Ham, juzi Jumapili.

Pia David de Gea yuko huru kurudi baada ya kujitenga kwa muda, na United inaweza kuwa na wakati mzuri kwenye mchezo huo utakaopigwa katika dimba la San Siro, baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 1-1.

"Nina natumaini kuwa na wachezaji wanne au watano kwenye mchezo huo," alisema Solskjaer baada ya kushinda dhidi ya West Ham.

"Tuna matumaini kwamba, inawezekana Edinson na Anthony kuwa fiti. Donny, pia natumaini atakuwa fiti. Huku pia Paul anaweza kuwa fiti pamoja na kurudi kwa David."

## SHAQIRI: ANFIELD SASA NI RAHISI KWA TIMU NDOGO

**LIVERPOOL, England**

XHERDAN Shaqiri amesema kwamba, kwa sasa mechi inayochezwa katika dimba la Anfield ni "rahisi" kwa klabu ndogo tu na anakubali Liverpool wanateseka kwa kukosa mashabiki wao.

Mabingwa hao wa msimu uliopita wa Ligi Kuu Kuu, wameruhusu kuachia taji bila kujitahidi msimu huu wa 2020-21, wakipoteza michezo tisa na sare saba na kuwa nyuma kwa alama 28 dhidi ya vinara, Manchester City.

Sita kati ya hizo wamefungwa pale Anfield, na Shaqiri amekubali kwamba 'Wekundu' hao hawana nguvu kama ya zamani kwenye uwanja wa nyumbani na 'wamemisi' sapoti ya mashabiki wao, ambao bado hawawezi kuhudhuria mechi kutokana na janga la corona.

"Kila mtu anajua jinsi mashabiki wetu wakiwapo wakati wa mechi wanavyotusukuma," alisema winga huyo wa Uswisi akiiambia Sky Sports.

"Kila mtu anajua ni michezo mingapi tumeweza kurudi ikiwa tutafungwa bao.

"Nadhani kuna michezo mingi ambayo unaweza kuona hiyo. Kwa kweli, tunawakumbuka sana.

"Kwa timu ndogo, ni rahisi kufika Anfield bila mashabiki. Hakuna shinikizo. Unaweza kuona hivyo kwa njia nyingi na katika michezo mingi. Timu ndogo tunakuwa na nafasi zaidi ya kushinda."

Liverpool ya Klopp jana Jumatatu ilikuwa inaivaa Wolves kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

# Arsenal haijakata tamaa EPL kufuzu UEFA – Arteta

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema 'Washikabunduki' hao bado wanakodolea macho kumaliza kwenye nne bora Ligi Kuu England ili kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kupata ushindi dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la London, Tottenham Hotspur.

Penalti ya kipindi cha pili ya Alexandre Lacazette iliisaidia Arsenal kuifunga Tottenham 2-1 Jumapili wakati Arteta akisherehekea ushindi wake wa kwanza wa mchezo wa ligi dhidi ya Spurs tangu achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo.



Bao la Erik Lamela liliwaweka mbele Tottenham kabla ya Martin Odegaard kuisawazishia Arsenal.

Kiungo wa Tottenham, Lamela akajikuta akiipa pigo timu yake wakati alipotolewa kwa kadi nyekundu dakika ya 76 baada ya Lacazette kufunga la pili.

Arsenal ipo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England ikipitwa pointi 10 kutoka kwenye nne bora, huku zikiwa zimebaki mechi 10 ligi kufikia mwisho.

Lakini Arteta bado hajakata tamaa na matumaini ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

"Ukiangalia kimahesabu unaweza kuona haiwezekani, lakini tunaamini tunaweza kwa uhakika kabisa," alisema Arteta, ambaye alichukua mikoba ya Unai Emery Desemba mwaka 2019, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunajua kwamba, tunatakiwa kuendelea kuwa kwenye kiwango bora, kuwa na nafasi katika mechi zote za mbele yetu.

"Lakini tutapambana na kuhakikisha tunajaribu kwa kiwango kilekile kwenye kila mchezo."


Arsenal haijacheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2016-17 na imekuwa ikishiriki kwenye Ligi ya Europa kwa misimu minne iliyopita.

## MOUNRINHO AWANYOOSHEA KIDOLE BALE, NDOMBELE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amewataja Gareth Bale na Tanguy Ndombele kuwa walikosa uimara baada ya Tottenham kukubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Arsenal, Jumapili.

Spurs walianza kuongoza kwa bao la Erik Lamela, ambaye baadaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu.



Lakini bao la Martin Odegaard ambalo ni la kwanza kwenye Ligi Kuu England likawarudisha mchezoni Arsenal, kabla ya Alexandre Lacazette kufunga la ushindi dakika ya 64 kwa mkwaju wa penalti.

Bale aliingia kwenye mchezo huo tayari akiwa na mabao sita na pasi za mwisho tatu kutoka mechi saba zilizopita kwenye mashindano yote, lakini hakupiga hata shuti moja au pasi muhimu, kabla ya kutolewa na nafasi yake kuchukuliwa na Moussa Sissoko dakika ya 57.

Dakika tano baadaye, Ndombele ambaye naye hakuwa na mchango kwenye mchezo huo akatolewa na nafasi yake kuchukuliwa na Dele Alli.

"Gareth na Tanguy, walihitaji uimara na nguvu zaidi kwenye mchezo ule. Tulihitaji kuwa na pasi nyingi zaidi," alisema Mourinho baada ya mchezo huo.

"Tulimhitaji mapema zaidi Sissoko, kwani alipoingia alionyesha nguvu na utofauti mkubwa kwenye nafasi ya kiungo tofauti na Tanguy.

"Halafu Dele alikuwa mchezaji ambaye tulimhitaji, kwani alikuwa vizuri na alielewana sana na Harry."

## DE LIGT ATUA RADA ZA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER imerudi tena kwenye mbio zake za kuwania kumsajili mlinzi wa kati, Matthijs De Ligt, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

De Ligt mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa anakipiga kule Juventus, ameingia kwenye rada za 'Mashetani Wekundu' hao baada ya kumkosa mara ya kwanza.

Iliripotiwa kwamba, Man United walikuwa wanawanyatia Sergio Ramos au Rapahel Varane wa Real Madrid, lakini sasa wameamua kurudisha nguvu zao kwa De Ligt.

Awali, United ilishindwa kumnasa De Ligt alipokuwa Ajax baada ya mchezaji huyo kuamua kutua Juve mwaka 2019, lakini hadi sasa bado anahaha kujihakikishia namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Na Man United wanataka kutumia udhaifu huo kwa kumhakikishia "maisha mazuri" pale Old Trafford.



# ZAHA

## AWEKA HISTORIA YA KUTOPIGA GOTI

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, amekuwa mchezaji wa kwanza wa Ligi Kuu England kukataa kupiga goti kabla ya kuanza kwa mechi.

Zaha alisimama katika mechi waliyopata ushindi dhidi ya West Brom, Jumamosi, kitendo anachotarajia kitaonyesha kwamba, nguvu zaidi inahitaji kufanywa kupambana na ubaguzi wa rangi.

Katika taarifa yake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alisema, "Nitaendelea kusimama na sitafuata tena mpango uliopitishwa kwenye ligi msimu uliopita."

Wachezaji wa Ligi Kuu England walianza kupiga goti kabla ya kuanza kwa mchezo kuunga mkono harakati ya maisha ya watu weusi, baada ya kifo cha George Floyd huko Marekani Mei, mwaka jana.

"Uamuzi wangu wa kusimama kabla ya kuanza kwa michezo umekuwa wazi kwa umma kwa wiki kadhaa sasa," Zaha alisema.

"Hakuna uamuzi sahihi au mbaya, lakini kwangu mimi binafsi nahisi kupiga magoti imekuwa sehemu tu ya utaratibu wa kabla ya mechi na kwa sasa haijalishi ikiwa tunapiga magoti au tunasimama, wengine wetu bado tunaendelea kubaguliwa."

Mchezo dhidi ya West Brom ulikuwa nafasi ya kwanza kwa Zaha kutoa maoni yake baada ya kupona jeraha la nyama ya paja.

Zaha raia wa Ivory Coast sasa ameungana na klabu za Daraja la Kwanza, Derby Country, Bournemouth na Brentford kwa kutoshiriki tena kwenye harakati hizi za kupiga goti.

Mkurugenzi Mtendaji wa Ligi Kuu England, Richard Masters, amesema kupiga goti kutaendelea hadi mwisho wa msimu, lakini kutakuwa na mazungumzo mapya na wachezaji juu ya njia bora zaidi.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PELE AMPA TANO CR7 KUVUNJA REKODI YAKE

Maisha ni safari ya peke yako, kila mmoja anatengeneza safari yake, hongera kwa kuvunja rekodi yangu ya...

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

PELE amempongeza Cristiano Ronaldo baada ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ureno kufunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Cagliari na kuivunja rekodi yake kwa idadi ya mabao aliyofunga kwenye mechi rasmi.

Ronaldo alifunga mabao hayo matatu ndani ya dakika 32 za mwanzo na kumfanya afikishe jumla ya mabao 770 - matatu zaidi ya Pele, aliyefunga mabao 767.

Baada ya Ronaldo kufikisha idadi hiyo ya mabao Pele aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kumpongeza.

"Maisha ni safari ya peke yako. Kila mmoja anatengeneza safari yake. Na safari nzuri unayokuwa nayo mwenyewe. Navutiwa sana na wewe, napenda kutazama ukicheza na hii si siri kwa mtu yeyote.

"Hongera kwa kuvunja rekodi yangu ya mabao niliyofunga kwenye mechi rasmi," aliandika Pele.

Baada ya mchezo huo dhidi ya Cagliari, Ronaldo naye alielezea kupitia ukurasa wake wa Instagram kwa nini sasa anaitambua "rekodi".

"Wiki chache zilizopita kulikuwa na habari kwamba mimi ni ndiye mfungaji bora katika historia ya soka, nikipita mabao rasmi ya Pele 757," alisema.

"Ingawa nashukuru kwa kutambua ile rekodi, sasa ni muda wangu kuelezea kwa nini sikuitambua rekodi ile tofauti na sasa.

"Leo nimefikisha mabao rasmi 770 katika maisha yangu ya kucheza soka, maneno yangu ya kwanza yanaenda kwa Pele.

"Hakuna mchezaji duniani ambaye tangu tunakua habari zake kwenye soka na mabao yake tumekuwa tukisimuliwa na kuangalia kama Pele.

"Najisikia furaha kubwa kwa sasa mimi kutambulika kama mfungaji bora duniani, kwa kuipiku rekodi ya Pele, sikuwahi kufikiria hilo hata siku moja wakati nikiwa mtoto nakua kule Madeira."

## KWA UFUPI

### AGUERO ANUKIA BARCA
BARCELONA wanakaribia kufikia mkataba wa kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, lakini uhamisho wa bure wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, utategemea ikiwa klabu hiyo ya Nou Camp itafanikiwa kumshawishi Lionel Messi mwenye miaka 33, kubaki. ***(AS)***

### SOLSKJAER KUUZA WANNE
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, huenda akawauza wachezaji Jesse Lingard mwenye miaka 28, Juan Mata (32), Diogo Dalot (21) na Phil Jones (29), ili kuongezea bajeti yake ya usajili ya pauni milioni 80. ***(Metro)***

### CITY WAMWINDA MENDES
MANCHESTER City wamewasiliana na Sporting Lisbon kuhusu mlinzi wao, Nuno Mendes wanapojiandaa kuitangulia Real Madrid katika mbio za kumsajili nyota huyo raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 18. ***(AS, via Mail)***

### ARSENAL YAMTAKA N'DICKA
ARSENAL wanamtaka mlinzi wa Eintracht Frankfurt, Mfaransa Evan N'Dicka mwenye umri wa miaka 21, na wameomba kupewa maelezo kuhusu hali ya kiungo wa kati wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye miaka 24. ***(Express)***

### MARTINEZ NA MKATABA MPYA
MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23, anaamini kuwa atasaini mkataba mpya na klabu hiyo, licha ya kile Muargentina huyo alichotaja kuwa "changamoto kidogo za kifedha" zinazokabili klabu hiyo ya Italia. ***(Sky Sports Italia, via Goal)***

### ERIKSEN ABADILI MAWAZO
CHRISTIAN Eriksen alikuwa amehusishwa na tetesi za kuondoka Inter Milan Januari, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, amesema anafurahi kuwa katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Sky Sports Italia, via Football Italia)***

### EMERSON AWINDWA CHELSEA
CHELSEA inahitaji angalau euro milioni 20 kumpata mlinzi wa Italia, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26, lakini Inter Milan na Napoli pia zinataka kumsajili. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

### RONALDO YUPO SANA JUVE
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri wa miaka 36, amesema majaliwa yake yapo Juventus, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa miamba hao wa Serie A, Fabio Paratici. ***(ESPN)***

### JOTA AKARIBIA LIVERPOOL
WOLVES itapata pauni milioni 12 kutoka Liverpool kipindi cha majira ya joto ikiwa ni sehemu ya dili la mshambuliaji wa Ureno, Diogo Jota mwenye umri wa miaka 24, kujiunga na Anfield. ***(Telegraph - subscription only)***

### PULISIC KUBAKI CHELSEA
KIUNGO wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, ambaye anahusishwa na kuwaniwa na Manchester United na Liverpool, anataka kupigania namba Chelsea. ***(Fabrizio Romano via Express)***

### MORIBA NUSURU ATUE CITY
BABA wa kinda wa Barcelona, Ilaix Moriba, amesema alifuta safari ya mwanawe huyo kwenda Manchester wakati nyota huyo mwenye umri wa miaka 18, alipokaribia kujiunga na Manchester City mwaka 2019. ***(Sport)***

## HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAPANIA TATU ZA PYRAMIDS KWA MKAPA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Moroco, amesema wana kila sababu ya kupambana na kufanya vizuri katika michezo ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF) wakianza na mechi ya kesho dhidi ya Pyramids ya Misri, kwa kuwa timu nyingi kwenye michuano hiyo hutumia vizuri viwanja vya nyumbani kupata pointi.

Namungo FC ambayo mechi yake ya kwanza ugenini nchini Morocco ilipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Raja Casablanca, inatarajia kuikaribisha Pyramids katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho baada ya ule waliouzoea wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Dar es Salaam kufungiwa na CAF.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Moroco alisema wanaendelea vizuri na wachezaji wake wote wako fiti na tayari kwa ajili ya kupambana kupata matokeo mazuri katika ardhi ya nyumbani kesho.

Alisema amefanikiwa kuwaona wapinzani wao, Pyramids dhidi ya Nknana FC, kwa na kubaini udhaifu na ubora wao, hivyo kufanyia kazi kikosi chake ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mchezo huo.

"Ni mechi ya ushindani mkubwa ukizingatia wenzetu ni wazoefu wa michuano hii, wana kila kitu katika mpira, kwa upande wetu tunamejiandaa kupambana kutafuta matokeo katika uwanja wetu wa nyumbani maana katika michuano hii kila mmoja anashinda kwake," alisema Moroco.

Alisema baada ya kuuona ubora wa Pyramids, katika kila idara ndani ya uwanja, atahakikisha anaingia kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu wapinzani wao hao ili kupata matokeo mazuri.

"Hadi sasa sina mchezaji majeruhi wote wako fiti, jambo zuri ni kuwapo kwa wachezaji wetu Abdulhalim Humud na Lucas Kikoti ambao katika mechi ya Morocco hawakucheza," alisema kocha huyo.

Alisema ana imani mechi yao dhidi ya Pyramids watafanya vizuri kwa kupata matokeo chanya kwa sababu kurejea kwa baadhi nyota wake hao, na mchezaji pekee atakayemkosa akiwa ni Haruna Shamte aliyeonyeshwa kadi nyekundu katika mchezo uliopita dhidi ya Raja Casablanca.

Namungo ambayo ipo Kundi D katika michuano hiyo pamoja na Nkana FC ya Zambia, katika mchezo wa awali ilipoteza kwa penalti iliyofungwa na Soufiane Rahimi dakika 54 kwa mkwaju wa penalti.



Kikosi cha Namungo FC kinachoshiriki michuano ya CAF, ambacho kesho kitakuwa na kibarua kigumu Uwanja wa Benjamin Mkapa kitakapoikaribisha Pyramids ya Misri. **PICHA: MAKTABA YETU**

## Azam yageukia washambuliaji

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema utatumia vizuri wiki tatu za mapumziko ya kupisha kalenda ya kimataifa kwa timu za taifa, kwa kuendelea na mazoezi huku wakiwaandalia programu maalum washambuliaji wa timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati, alisema walikuwa wanafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika michezo iliyopita ikiwamo safu ya ulinzi kuruhusu mabao na sasa wako kwa washambuliaji kuhakikisha wanatumia vizuri nafasi wanazotengeneza uwanjani.

Alisema wachezaji wanafanya kazi nzuri ila kwa sasa wanahitaji kuimarisha safu ya ushambuliaji kwa sababu wana imani nafasi wanazotengeneza kama wataweza kuzibadili kuwa mabao watakuwa wakipata ushindi mkubwa mechi zijazo.

"Tulikuwa na shida kwenye safu yetu ya ulinzi kwa kuruhusu mabao, hilo tumelifanyia kazi na liko sawa, sasa hivi nguvu zetu ni katika safu ya ushambuliaji, tumekuwa tunatengeneza nafasi nyingi muhimu lakini hazifanyiwi kazi.

"Tuna imani katika mapumziko haya yatatusaidia kufanyia kazi na kuweka sawa tatizo hilo kwa kuwapa programu muhimu ili mechi zitakaporejea tuwe vizuri katika nafasi hiyo," alisema Vivier.

Alisema ushindani wa Ligi Kuu ni mkubwa na ana imani hatua kwa hatua wachezaji wao wanazidi kuimarika na kuleta ushindani ndani ya ligi hiyo, kwa kupata matokeo chanya na kufikia malengo ambayo wamejiwekea.

Azam FC kwenye msimamo ipo nafasi ya tatu baada ya kujikusanya pointi 44 zilizotokana na mechi 24 ilizocheza hadi sasa wakati huu Yanga ikiwa kileleni na alama zake 50 zikitokana na mechi 23 huku nafasi ya pili ikiwa mikononi mwa mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 46, lakini wakiwa nyuma michezo mitatu.

# Chama, Miquissone bado vinara wa 'asisti' Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imefikisha jumla ya raundi 24, wachezaji wawili wa Simba, Clatous Chama na Luis Miquissone, wameendelea kuwa vinara wa kutoa pasi za mabao (assist), huku timu yao ikiwa bado ina viporo vitatu.

Hadi kufikia Februari 24, mwaka huu, wachezaji hao kila mmoja tayari ameshatoa pasi za mwisho tisa zilizozaa mabao, wakiisaidia timu yao kuwa kwenye nafasi ya pili mpaka sasa kwa pointi 46.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Chama raia wa Zambia na mwenzake Luis kutoka Msumbiji, wanawakimbiza wachezaji mbalimbali kwa kutoa pasi nyingi zilizozalisha mabao, ambapo wawili hao pekee, wametoa pasi zilizozaa mabao 18 kati ya 46 ambayo yameshafungwa na timu hiyo.

Kwa muda mrefu Ligi Kuu, wachezaji hao wameendelea kuwa vinara, lakini safari hii nafasi ya pili ikichukuliwa na beki wa Kagera Sugar, David Luhende ambaye yeye ana 'assist' saba, pamoja na timu yake kuwa hoi bin taaban.

Dickson Ambundo wa Dodoma Jiji anakamata nafasi ya tatu kwa 'assist', yeye akiwa na sita, lakini akiwa pamoja na Rajab Athumani wa Gwambina FC.


Wachezaji ambao wamefikisha pasi za mwisho tano kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ni Mzimbabwe Prince Dube wa Azam FC, Idd Selemani 'Nado' pia wa Azam, Abdulrahman Mussa wa Ruvu Shooting na Danny Lwanga wa JKT Tanzania.

Winga wa Yanga, Tuisila Kisinda, anawaongoza wenzake ambao wameshatoa 'assist' nne mpaka sasa kwenye ligi. Mkongomani huyo, yupo pamoja na mchezaji mwenzake wa Yanga, Mburkina Faso, Yacouba Songne, Nzigamasambo Styve, Mrundi anayeichezea Namungo, Isael Mwenda wa KMC, Ramadhani Chombo 'Redondo' wa Azam na Never Tegere, Mzimbabwe anayeichezea Azam FC.

Michezo

Jumanne Machi 16, 2021

Nipashe



PELE AMPA TANO CR7 KUVUNJA REKODI YAKE

HABARI UK 22

WATATOKAJE?...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (mbele), akiwa mazoezini pamoja na wenzake kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al-Merrikh itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. PICHA: SIMBA

## MWAMBUSI KUAMUA UBINGWA YANGA SC

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya Juma Mwambusi awali kusema kwa sasa hawezi kuzungumzia suala la ubingwa kwani cha muhimu kwao ni kupambania timu hiyo kupata matokeo mazuri katika kila mechi, ni wazi neno "ubingwa" anatakiwa kuamua moja kulitoa ama la, baada ya kukabidhiwa rasmi mikoba ya kuinoa timu hiyo hadi mwishoni mwa msimu.

Mwishoni mwa wiki Mwambusi alimwambia mwandishi wetu kuwa, hawezi kuzungumzia suala la ubingwa ila anachotaka ni kujenga timu ya kupambania matokeo katika kila mechi, lakini baada ya kauli hiyo uongozi wa Yanga ulitangaza rasmi kumpa mikoba ya ukaimu kocha mkuu hadi mwishoni mwa msimu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema Kamati ya Utendaji ya Yanga iliyokaa juzi, imeamua Mwambusi kukifundisha kikosi cha Yanga hadi Ligi Kuu ya msimu huu itakapomalizika, ndipo mambo mengine yaendelee.

Awali, Mwambusi alipewa timu kwa muda kukaimu, huku kukiwa na mpango wa kumleta kocha mkuu kipindi hiki hiki kabla ya ligi kumalizika.

"Kamati ya Utendaji imekaa, imeamua kuwa Mwambusi atabaki na kikosi hadi mwishoni mwa msimu na amepewa nafasi ya kuchagua kocha msaidizi, na wasaidi wengine kwa siku hizi mbili," alisema Bumbuli.

Alisema kutokana na hali hiyo, mchakato wa kusaka kocha mpya, utaendelea, lakini si kwa kasi kama ile ya kwanza, badala yake kwa sasa watauendesha taratibu na makini zaidi.

# SIMBA: MERRIKH HAWATOKI LEO

## Gomes asema ushindi lazima, Lwanga ndani, CAF yaruhusu Wasudan waliozua utata kucheza, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, leo wataweka historia nchini, watakapoivaa Al-Merrikh ya Sudan kwa mara ya kwanza bila mashabiki kwenye mechi ya raundi ya nne ya michuano hiyo hatua ya makundi.

Simba itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikicheza bila mashabiki baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuamua hivyo muda mfupi tu baada ya uongozi mpya kuchaguliwa.

Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes da Rosa, amesema anasikitika kuwakosa mashabiki kwani wamekuwa ni muhimu na aliwaona siku ya mechi dhidi ya Al Ahly walipotoa mchango mkubwa wa kuondoka na pointi tatu kwenye mechi hiyo, Februari 23, mwaka huu, wakishinda bao 1-0, lakini akaongeza kuwa wako tayari kupambana kwenye mazingira yoyote yale.

"Lazima tushinde, ni muhimu sana kupata alama tatu kesho kwa sababu kwenye hili kundi ili kufika robo fainali tunahitaji alama 11, hivyo ni muhimu sana kushinda. Kwa nilichokiona kwenye mazoezi kwa siku hizi tupo vizuri," alisema kocha huyo.

Kwenye mechi ya leo, Simba itamkosa beki wake tegemeo Pascal Wawa, huku Gomes akisema kiungo wake mkabaji, Taddeo Lwanga, ambaye mashabiki wengi walikuwa na wasiwasi ya kuukosa mchezo huo, anaweza kuwamo dimbani kama kawaida.

Kuhusu hilo, kocha Gomes alisema hana wasiwasi nalo kwa sababu Simba ina mabeki wengi ambao wanaweza kucheza nafasi ambazo zimeachwa wazi kama Peter Muduhwa, Erasto Nyoni, Kennedy Juma na wengineo.

"Tadeo (Lwanga) anaweza kucheza, Wawa (Pascal) ndio mchezaji ambaye atakosekana kwenye mchezo wa leo, lakini tunao wachezaji wengine wazuri ambao wanaweza kucheza nafasi yake kama Peter, Kennedy ama Erasto ambaye ana uzoefu mkubwa," alisema.

Naye Nahodha wa kikosi hicho, John Bocco alisema kuwa wapo tayari kupambana ili mradi tu zipatikane pointi tatu.

"Tupo nyumbani na tupo tayari kupambana kwa ajili ya timu na kupata alama tatu. Tunashukuru kwa ushirikiano tunaopata kwa mashabiki ingawa tunajua kwamba kesho hawatakuwapo uwanjani, lakini tunaamini kwa dua zao tutapata ushindi," alisema Bocco.

Timu hizo zilipokutana nchini Sudan, Machi 6, mwaka huu, zilimaliza dakika 90 kwa sare tasa kwenye mechi hiyo ya Kundi A ambalo Simba ipo kileleni ikiwa na pointi saba ikifuatiwa na AS Vita na Al Ahly zenye pointi nne kila moja, ambazo nazo zitakuwa uwanjani nchini DR Congo leo. Al-Merrikh ipo mkiani ikiwa na alama moja.

Katika hatua nyingine, CAF imeruhusu wachezaji wa Al-Merrikh, Ramadan Agab na Bakhit Khamis kucheza mechi dhidi ya Simba.

Awali, Simba iliiomba CAF kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za wachezaji hao kufungiwa na Shirikisho la Soka la Sudan kwa kipindi cha miezi sita, lakini wakacheza mchezo dhidi yao nchini Sudan.

Lakini kwa mujibu wa CAF, wachezaji hao walifungiwa kucheza mashindano ya ndani, na kifungo chao hakihusiani na kushiriki mashindano ya CAF.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042